



AL- WAHDA

UMOJA WA WAISLAMU

Mwandishi:
Seyyid Murtadha Al-Ridhwani

Mtarjumi:
Abdallah Mohamed

**Haki ya kunakiki imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION**

ISBN: 978-9987-427-28-4

Mwandishi:
Sayyid Murtadha Al-Ridhwani

Mtarjuma:
Abdallah Mohamed

Mhariri:
Dr. M. S. Kanju

Kupangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Agosti 2006 - Nakala 1000
Toleo la Pili: Juni, 2017 - Nakala 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation
P O Box 19701
Dar-es salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
E-mail: alitrah@yahoo.com
Website: www.alitrah.info

YALIYOMO

Utangulizi wa Mwandishi.....i	
Abbas Tarjummani Muhammad Al-Madani	
Kujenga umoja wa Kiislamu.....ii	
Hitilafu zilizopo.....2	
Sheikh Mohamed Al-Ghazali	
Umoja wa Kiislamu.....5	
Muhammad Farid Al- Ghazaly	
Mwito wa kuwa kitu kimoja.....7	
Mshikamano wa Kiislamu.....12	
Muhammad Shaltut Abdul-Hadi Masud Al- Ibyari	
Mahojiano.....27	
Muhammad Al-Faham Abdur-Rahman An-Najjar	
Mahojiano kati ya mtunzi na mkuu wa msikit wa cairo.....31	
Barua ya Sheikh. Ahmad Hasan Al-Barqi.....33	
Ust. Abdul-Fataha Abdul maaqsud	
Historia ya Kiislamu.....34	
Dkt. Hamid Hafna Daud	
Baina ya Shia na Sunni.....35	
Dkt. Suleiman Duniya	
Wanahistoria hawana usawa kwa Shia.....37	
Dkt. Hamid Hafna Daud	

Shia na Fiqh ya Kiislamu.....	43
Abdul-Wahab Abdul-Latif	
Hapana tofauti kubwa.....	44
Ni tawi.....	46
Kuhusu Fiqh.....	47
Ali bin Abi Talib.....	50
Sifa zake.....	52
Bado tupo na Ali.....	55
Wastashirikina na Ukoloni.....	60
Dkt. Abul-Wafaa Al- Ghanimi Attaftazani	
Dkt. Hafna Daud	
Nia yao ni kutia shaka.....	64
Ndoa ya <i>Mut'a</i> katika Uislamu.....	65
Abdul-Hadi Mas'ud	
Maswahaba wa mtume (s.a.w.).....	72
Dkt. Hamid Hafna Daud	

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiaarabu kilichoandikwa na Mwanachuoni: Sayyid Murtadha Al-Ridhwani.

Kitabu hiki kinahusu umoja wa Waislamu, mada ambayo ni muhimu sana tokea zamani, na ambayo umuhimu wake umezidi sana katika zama hii tuliyo nayo sasa. Maadui wa Uislamu wametangaza wazi wazi kwamba: sasa baada ya kuusambaratisha ukomunisti, adui yetu aliyebacki ni Uislamu na Waislamu. na wote tumeona walivyofanya na wanavyoendelea kufanya katika nchi za Kiislamu, nenda Afghanistan angalia walivyofanya, nenda Iraq angalia walivyofanya, nenda Pakistan angalia wanavyo wagombanisha Waislamu kule kwa kuzikuza tofauti za Madhehebu. Sasa hivi wameiandama Iran, kisa, Iran wanataka kutengeneza nishati ya nyukilia kwa matumizi yao ya viwanda na matumizi mengine ya kawaida (sio kwa ajili ya silaha), lakini wimbo unaoimbwa na maadui hawa ni kwamba Iran wanataka kutengeneza silaha za maangamizi. Ajabu ni kwamba wamesahau silaha za maangamizi walizonazo wao na ambazo wamezitumia huko Hiroshima Japan na kuteketeza maelfu ya watu, na athari yake inaendelea mpaka leo. Ukweli ni kwamba Maadui hawa hawataki kuona Waislamu wanaendelea katika nyanja yoyote ile, kwa hiyo wanatumia kila hitilafu tulizo nazo ili kutusambaratisha. Na kwa kiasi fulani wamefanikiwa, na kama hatutanabahi basi hali itakuwa mbaya zaidi upande wetu Waislamu, ni muhimu hilo kulitambua.

Mwandishi wa kitabu hiki amekusanya maoni ya wanachuoni wakubwa wa Sunni na Shia, na wote wamesisitizia juu ya umoja wa Waisalamu bila kujali Madhehebu zao. Ili kuweza kukabiliana na maadui hawa, hatuna budi sisi kufuata ushauri wao.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni njia ya kujuana sisi Waislamu na kufuata maneno ya Allah swt. "**Shikamaneni nyote katika kamba ya Allah kwa pamoja wala msi-farikiane.**" Na kwa hakika hakuna kitakachotufanya tumshinde adui yetu ila Umoja na kuachana na kasumba za kimadhehebu.

Tumeona tukitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, ili wasomaji wetu Waislamu wanaotumia lugha hii waweze kuchangia katika mada hii muhimu.

Tunamshukuru Ndugu yetu **Ustadh Abdallah Mohamed** kwa kukubali kukifanyia tarjuma kitabu hiki, na wale wengine wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation

UTANGULIZI WA MWANDISHI

Baadhi ya waumini wema na wenyе nia nzuri na wanao-jishughulisha kuondoa hitilafu zilizoko miongoni mwa umma wa Kiislamu wameniomba nikusanyе maoni ya baadhi ya waandishi wa kisasa kuhusu umoja wa umma wa Kiislamu ili kutekeleza kauli ya Mwenyezi Mungu: “**Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakane.**”

Vilevile kujiepusha na mizozo kwa kauli yake Mwenyezi Mungu: “**Wala msizozane mtafeli ...**”

Katika hali kama hizi za sasa za kiubaguzi, yapasa Waislamu wote wawe bega kwa bega, wawe kitu kimoja na wafanye juhudи za kuungana na kuwe na sauti moja ili lao liwe moja dhidi ya watu wengine.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema: “**Hakika umma wenu huu ni umma mmoja na Mimi ni Mola wenu basi niabuduni**”

Ikiwa madhehebu nyingine potofu hivi leo zinaungana kwa wingi, kwa nini basi sisi Waislamu tusiwe na umoja na tusihurumiane?

Mtume (s.a.w.) anasema: “**Mfano wa Waislamu katika kuden-dana kwao na kusikitikiana ni kama mfano wa mwili mmoja, iwapo kiungo kimoja cha mwili huo kitaumwa basi viungo vingine pia vitaumwa huku vikikesha na vikiwa na homa.**”

Kwa hivyo basi yapasa Waislamu wote waelekee kwenye kuwa kitu kimoja na kuwa na sauti moja, kwani Mwenyezi Mungu ame-tuambia kutupa nusra yake pale aliposema:

“Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atawanusuru na kuwaimarisha.”



Twamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu ayaelekeze kwenye mambo yaliyo na kheri kwa umma wa Kiislamu, tuishilie kwenye mafarakano na atuwafikie kwa yale yaamrishwayo.

KUJENGA UMOJA WA KIISLAMU (*AL-WAHDA*)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) amesema:

﴿ قَدْ حَلَّتْ مِنْ قَبْلِكُمْ سُنُنٌ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوْا كَيْفَ

كَانَ عَيْقَةُ الْمُكَدِّبِينَ ﴾

﴿ هَذَا بَيَانٌ لِلنَّاسِ وَهُدًى وَمَوْعِظَةٌ لِلْمُتَّقِينَ ﴾

“Zimepita adabu namna kwa namna walizotiwa waliokuwa kabla yenu. Basi safirini katika nchi na muone ulikuwaje mwisho wa waliokadhibisha. Haya ni maeleo yaliyo wazi kwa watu wote na uongozi na mauidha kwa wamchao. (3:137-138).

Kwa kipindi kirefu kilichopita moto wa chuki umechochewa baina ya Waislamu ili kuleta hitilafu kati yao, na hilo ni kwa kuwashughulisha na tofauti ndogondogo kwanza, ndipo wenye roho dhaifu wakanunuliwa na kuzitumia kalamu zao kuvunja umoja wa kiislam, wakadhaniana vibaya Waislamu wenyewe kwa wenyewe hata kufikia kukufurishana na kumwaga damu zao.

Bado akili hazijasahau mauaji na fitina zilizotokea kati ya Shia na Sunni nchini Iraq na Afrika ya Kaskazini katika enzi ya utawala wa Bani Abbas mpaka kuishia kwa dola ya Fatimiya.

Mimi naamini kwamba yote hayo yametokea kwa ajili ya kutaka

radhi ya Mwenyezi Mungu tu, na kwa sababu vikundi vyote viwili hivyo vinaona kuwa kila kimoja kiko kwenye haki na kingine kimepotoka, na hivyo damu ya nduguye Mwislamu ni halali kwake bila ya kuhisi kuwa huyo ni nduguye, “Je siwaambii wale waliohasirika? Hao ni wale ambaao amali zao zimepotea katika maisha ya duniani na wao wanadhani kuwa wanafanya mema.” na yote hayo ni kwa sababu ya upotoshaji wa habari kutoka kwa wale wanaonufaika na mfarakano wa Waislamu.

Mfano wa wanavyuoni hao wamekuwa kama kasuku wanakariri kile wanachoambiwa na mawakala wa utawala bila ya kuhakikisha au kuchunguza, na wanasahau kwamba yale wanayoandika hayaendi na wakati wa sasa ambaao haukubali jambo kiholela tu bila ya kuthibiti ukweli wake, na ukweli wa hayo niyanenayo umekusanywa na mwanachuoni Seyyid Murtada Ridhaa aliyejitelea nafsi yake kwa bidii zote ili kuueneza ukweli wa Kiislamu, kuhakikisha umoja na kuunganisha Waislamu.

Na haya tuyasomayo katika kitabu hiki ni natija ya juhudi za wanavyuoni katika kupekua, kuchunguza na kusoma vitabu vikubwa, ndipo kwa kuamua kusema ukweli kwa ushujaa wote na wakayaeneza ili wengine pia waelimike, huenda nyoyo zikakaribiana, ukaondoka na uchafu, na umma wa Kiislamu kurudi kama ulivyokuwa mwanzo umma bora ulioletwa kwa watu kama alivyosema Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

“Hakika umma wenu huu ni umma mmoja na Mimi ndiye Mungu wenu basi niabuduni.”

Basi maji na yarudi kwenye mapitio yake, na ndugu wa Kiislamu wapeane mikono Mashariki na Magharibi mwa dunia na waungane katika kuondoa tofauti za zamani, wafungue ukurasa mpya; suluhusheni baina ya ndugu zenu, ili wavishinde vitimbi vya maadui.

Vilevile mtazamo mmoja tu wa maneno ya wanavyuoni hao (yaliyomo kitabuni humu) yanayotokana na nasaha za Mwenyezi Mungu na Mtume wake (s.a.w.), unatosha kutambua hakika inayowapasa Waislamu wote waijue.

“Hakika hilo mna ukumbusho kwa mwenye kuwa na moyo au akatega sikio na hali anashuhudia.”

Abbas Tarjummani.

Tehran

16 Dhul-Hijja, 1398 A.H.



**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehma
Mwenye kurehemu.**

Bila shaka mambo ya umma wa Kiislamu hayawezi kusuluhihish-wa kwa kuendeleza usongo, hitilafu na kufufua mambo ya chuki yaliyopita siku za nyuma.

Je yafaa tuendeleze tofauti zetu baina ya Sunni na mwingine, au mjadala wa Mungu kuwa na mwili au hana, au wa Sunni na Shia.

Je tupoteze wakati na akili za wazee na vijana wetu juu ya mjadala wa kuwajibika au kutowajibika kwa Mungu? Au nadharia ya kuumba vitendo vyta waja? Au nadharia ya kufaa kumwadhibu mtii na kumlipa mema muasi na mengineyo? Hivi ulimwengu huu wa sasa unaoendelea kwa kasi utatungoja sisi tumalize tofauti zetu ndogondogo kama hizi?

Bila shaka jibu ni kwamba hapana nafasi ya jambo hilo, na ikiwa waliotutangulia walikuwa na wakati wa kufikiria hayo, sasa hivi sisi tu katika mazingira mengine, la muhimu ni kwetu sisi tuachane na tusahau kasumba hizi na tuseme tu kwamba sisi ni Waislamu, dini yetu ni moja, Mungu mmoja, Kitabu kimoja. Mtume wetu mmoja na malengo yetu katika maisha ni mamoja.

Aidha tujue kwamba maadui zetu ni wamoja, hawaangalii kuwa sisi ni Shia au Sunni bali hutuchukulia kuwa ni Waislamu, kinachotufanya tuwe wamoja ni malengo na misingi ya Uislamu.

Lengo letu sisi si Sunni au Shia aache madhehebu yake, la, bali tunachotaka ni wote waungane kwenye misingi inayoafikiana na

.....

watu, wasamehe katika mambo yasiyokuwa sharti mionganoni mwa masharti, wala nguzo mionganoni mwa nguzo za Kiislamu.

Na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwafiki na ndiye Mnusuru wa watu wenye nyoyo safi.

Muhammad Muhammad Al-Madani.

HITILAFU ZILIZOPO

Waislamu hawajahitilafiana kuhusu kwamba hukumu ni sehemu ya dini, yaani Uisalmu ni sharia na Imani; wala pia hawajahitilafiana kwamba Qur'an ndiyo inayohukumu.

Waislamu walichagua Maswahaba wale waliokuwa karibu zaidi na Mtume (s.a.w.), Shia wakaonelea kwamba Ali ndiye aliyefaa zaidi kwa ukhalifa, ambapo Makhawariji wanaonelea kwamba Mwislamu yejote afaa kufuatwa.

Je hitilafu hii inavunja misingi ya imani na mafunzo ya Sharia? Au ni mdahalo tu wa kisiasa uliowezekana kuzimwa kwa njia nyingi bila vita?

Vilevile Waislamu hawajahitilafiana kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwadilifu ambaye humlipa mema mtu mwema na kumwadhibu mwovu kama aliviyotuambia Mwenyezi Mungu katika Kitabu Chake kitukufu, na huo umekuwa ni wajibu wa kisharia kati ya Mu'tazila na Sunni.

Je kiakili hilo ni wajibu kwa Mwenyezi Mungu au la? Sasa, maswali kama hayo ni kupoteza wakati. Hitilafu hii yatokana na kukosa la kufanya; na haiwezekani kuwagawanya Waislamu kwa misingi ya maswali.

Ndipo tukasema kuwa hakuna tofauti zinazoweza kidini kugawanya Waislamu kama ulivyogawanyika mto Nile. Ndiyo, tunaweza kusema kuwa zipo madhehebu za kifikra au za ki-fiqhi; na hitilafu hizi ni mambo ya kisiasa yaliyobaki kwa hivyo yataonekana ni ya kawaida tu.

Mathalan, hivi sasa kuna upinzani mkali wa kisiasa uliogawanya Uingereza ambapo chama kimoja ndicho kinachotawala na vingine ni vya upinzani, je hali hii inamaanisha kuwa Uingereza imegawanyika mara tatu? La, sivyo.

Lau mazingira ya umma wa Kiislamu yangelikuwa mazuri magomvi yasingelikuwa makali kiasi hiki kilichoandikwa na Historia.

Pamoja na kutofautiana huko kwa maoni, ni lazima umma uwe na imani ya Kiislamu hata kama ni Mu'tazila au Khawariji au Shia. Dini ya Kiislamu inaamuru kuondoa mizozo na kushikamana kwa umoja, na ndiyo maana ya kauli yake Mwenyerzi Mungu **"Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyinyi nyote wala msifarikiane."**

Au kama Mtume (s.a.w.) alivyosema: **"Na msije mkawa makafiri baada ya kuondoka (kufariki) kwangu mkauwana nyinyi kwa nyinyi."**

Lakini sisi tumeyapinga maneno yote hayo tukafarikiana, tukazozana na tukapigana wenyewe kwa wenyewe kwa jina la dini kwa sababu tumefuata madhehebu mbali mbali, kila kikundi kinang'ania madhehebu yake na kuwapiga vita ndugu zake wengine Waislamu huku mfuasi wake akijidai kwamba yeze anainusuru dini hali ya kuwa anaiangusha kwa kuusambaratisha umoja wa Kiislamu.

Huyu hapa Msunni anapigana na Mshia, na Mshia anagombana na Msunni. Mshafi naye apigana na Mhanafi. Kisha kuna wale wanaowapiga vita watu wanaofuata njia za watu wema wa kale (Masalafi).

Je amri hii imetoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake au kutoka kwa Maimam Mujtahidina? Jibu ni hapana, isipokuwa ni ushindani tu na ugomvi ndio uliowapoteza njia iliyonyooka waka-fuata nyayo za shetani.

(Kitabu: *Ad-difaa'a'nil aqiida*)

Sheikh Mohamed Al-Ghazali.

Cairo, Misri. 1395. A.H.

UMOJA WA KIISLAMU

Mtume Muhammad (s.a.w.) alitambua kuwa kufaulu alikokukusudia Mwenyezi Mungu kwa ulimwengu hakupatikani ila kwa njia ya umma unaoamini kusimamia na kueneza dunia japokuwa kutakuwa na ugumu wa kupatikana kwake, ndipo akasema: "**Uislamu unahitajia zaidi umoja wa kijamii kuliko umoja unavyohitaji Uislamu.**"

Haya ni maneno yanayoonyesha mtazamo wa kina wa falsafa na kufanya mambo kwa pamoja. Mwanzo hakukuwa na falsafa hii, ndipo akaeleza umuhimu wake juu ya kujenga jamii ya pamoja ya Kiislamu kiasi kwamba isitengane mpaka litimie tangazo la neno la Mwenyezi Mungu dunia nzima, ndipo katika maneno yake Mtume (s.a.w.) akazungumzia udugu baina ya Waislamu mpaka wawe kama mtu mmoja, akasema: "**Mfano wa Waislamu katika kupendana na kuhurumiana kwao, ni kama mfano wa mwili mmoja, kiungo kimoja tu kikiuma basi viungo vingine pia vitashikwa na homa na kukesha.**"

"Asiyewashughulikia Waislamu si katika wao."

"Mwislamu kwa Mwislamu mwenzake ni kama majengo yanavyoshikamana."

"Hawezi kuamini mmoja wenu mpaka ampendelee nduguye lile analolipenda."

"Atakayetengana na jamii (ya Kiislamu) hata kwa shibri moja tu basi atakufa kifo cha ujahiliya."

Ilipokuwa hima ya Waislamu wa mwanzo ni katika ibada na kujiweka karibu na Mwenyezi Mungu, Mtume (s.a.w.) aliwabainishia kwamba kukesha kwa ajili ya kulinda jamii ya Kiislamu ni bora kuliko ibada zingine walizokuwa wakizitokuza, akasema, "**Mtu**

kumwangalia nduguye kwa pendo jema ni bora kwake kuliko kufanya itikafu mwaka mzima ndani ya msikitii wangu huu.”

“Mtu atakayekwenda kwa saa moja tu kwa ajili ya kumkidhia haja nduguye, iwe ni usiku au mchana, na hata asiweze kumtimizia basi huwa ni bora kwake kuliko kufanya itikafu miezi miwili.”

“Je siwapi habari juu ya lililo bora kuliko daraja ya Swala, Saumu na Sadaka?” Maswahaba wakamjibu, **“Kwa nini! Tuambie”** Mtume (s.a.w.) akasema: **“Ni kusuluuhisha walio-gombana.”**

Mtume (s.a.w.) hakuishia hapo bali aliwathibitisha kwamba kusuluhisha walio-gombana kwa ajili ya kujenga jamii, kunakinga na adhabu ya siku ya Kiyama, akasema: **“Mtu atakayewaondolea Waislamu kitu kinachowaudhi, Mwenyezi Mungu atamuandikia jema, na atakapoandikiwa jema ataingia Peponi.”** **“Mwenye kumfurahisha Mwislamu, Mwenyezi Mungu naye atamfurahisha siku ya Kiyama.”**

Mtume (s.a.w.) amesema: **“Watakapokutana Waislamu wawili wakapeana mikono hugawanywa misamaha sabini kati yao na sita huipata yule mwenye kuonyesha furaha zaidi.”**

Hadith zote hizi na nyininge kama hizi zimewafanya Waislamu kuwa kama mtu mmoja, na umma ukifikia hali hii ya kuwa na mpango mzuri na kusaidiana basi hauwezi kutetereka na matukio ya kawaida.

Kitabu: Dawaat Taqriib Uk. 343.

Muhammad Farid Wajdi.

Kimechapishwa Misri mwaka 1386 A.H

MWITO WA KUWA KITU KIMOJA

Kwa hakika nilihisi vibaya moyoni mwangu nilipokuwa nikisoma aliyoyaandika mzungu **Gould** juu ya Mshia na Msunni; je, ni kweli kuna Uislamu wa aina mbili kwenye umma wetu? La, Uislamu ni mmoja tu. Uislamu hauna mambo hayo yaliyooongezwa, yaliyozushwa. Mwenyezi Mungu alituridhia dini yetu kuwa ya Kiislamu na kwa karne sabini baba wa Mitume, Ibrahim, alituita hivyo.

Kisha akaja Mtume wa mwisho Muhammad (s.a.w.) akatuongoza njia na kututimizia neema na kutuachia *wahyi* na uongofu wake nasi tumeshikamana na turathi zake na hatutaki jengine. Ndiyo, Waislamu wametofautiana katika mambo mengi lakini alama yao wote ni ule ule Uislamu hawaridhii dini nyingine, kwa hivyo nini kimetokea?

Kwa kweli kuna watu hawamchi Mwenyezi Mungu katika dini yao na umma wao, wameacha mawingu mazito na wemejaza fikra za watu mambo mapotofu, watu wamekuwa ni wahanga wa uwongo usio na msingi, na siku kifunko kitakapofunguka na ukweli kujulikana wengi watadhihakiwa.

Ama mzungu **Gould** katika fikra zake anaona kwamba sisi tunajizamisha kwenye hitilafu bila ya sababu ya maana.

Siku moja alinijia bwana mmoja, katika watu wa kawaida huku akiwa amekasirika akauliza, “Vipi Sheikh wa Azhar ametoa fatwa kwamba Shia ni Madhehebu ya Kiislamu kama madhehebu mengine maarufu?”

Nikamuuliza, “Kwani waijua Shia?” Akajibu, baada ya kusita kidogo, “Ndio, wao ni watu wasio katika dini yetu.”

Nikamwambia: "Lakini nimewaona wakiswali na kufunga kama sisi." Yule bwana akastaajabu, akasema, "Vipi?" Nikamwambia "Basi la ajabu zaidi wao husoma Qur'an kama sisi, wanamtukuzu Mtume na wanaenda kuhiji Makka tukufu!" Akasema: "Lakini wao wana Qur'an nyininge na wanakwenda kwenye Al-Ka'aba ili watudhuru!"

Kwa hakika wengine katika sisi huwatafuta wengine ili kuwavunja kama Warusi wanavyofanyia Wamarekani na Wamarekani wanavyowafanyia Warusi, kama kwamba sisi si umma mmoja.

Ndiyo, sikatai kwamba zipo hitilafu baina ya baadhi ya wanavyuoni lakini haifai hitilafu hizo kuzihamishia kwenye medani ya maisha kwa ujumla na kuugawanya umma wetu na kuharibu mustakabali wake.

Hii ni kwa sababu wenyе malengo hayo wamefanya hivyo kitambobo sana ili umma upatwe na majanga kwa yule anayebaki na shari hii mpaka ifike mahali watu wengi waseme huu ni Uislamu wa Ki-sunni na huu ni wa Kishia.

Mwenyezi Mungu amlipe **Nadir Shah** kwa jihadi yake ya kuwaunganisha Waislamu, lakini Jumuiya ya *Daarul -Taqbir* ya zama zetu hizi inajaribu hilo kabla viongozi hawajaanza.

Ni kweli kwamba hitilafu zilianza za kisiasa zikapitia njia za viongozi, kwa hivyo hawa viongozi walioko sasa ni lazima watengeneze kile kilichoharibiwa na wenzao waliopita na watie nguvu zao katika kuunganisha. Lakini, kama nilivyosema, kazi hii hivi sasa ifanywe na Wanavyuoni. Yaani, ilimu ilikuwa imeathiriwa na utawala, na masomo ya dini yalitawaliwa na matakwa ya kidunia, kisha wale walionufaika na utawala wakaondoka wakabaki wasomi waliohadaika.

Kwa hivyo yatupasa sisi tunaoububa Uislamu tusahihishe makosa hayo na tuondoe vishawishi. Naamini fatwa ya Ustadhi mkuu **Sheikh Mahmud Shaltut** itaongoza kwenye njia hii nayo ni kufufua juhud za wale viongozi wenye *ikhlasi* na wasomi, na kukadhibisha mbegu za chuki zinazopandwa na wazungu.

Kwa maoni yangu fatwa hiyo ndiyo mwanzo wa njia na kufanya vitendo. Mwanzo wa njia ya kukutana chini ya nembo ya Uislamu aliotukamilishia na kuturidhia nayo Mwenyezi Mungu. Na ni mwanzo wa kufanya vitendo vya ujumbe unaowatukuza Waislamu.

Kuondosha dhana na uzushi kunahitajia wote, Sunni na Shia na kutengana mbali kunawaweka mbali na haki ya Mwenyezi Mungu na maisha ya dunia nayo yaenda mbio, na yule asiye na dini anapanda kwa haraka kuwakejeli wale watu walio nyuma, na hapana jingine kwa Uislamu ila kutibu maovu haya, lakini Uislamu upi? Ni ule Uislamu unaowafanya watu wawe ndugu? Je tuwashe moto uchome yai letu, na tujishughulishe na kulaumiana na kusema uongo?

Mimi naona njia bado ni ndefu lakini tumeshajua na tushaanza kwenda, na afuataye njia basi hufika. Mimi sisikitishwi na wale wanaojisemea ovyo tu, bali wanaoleta tuhuma wasiojali mwisho wa mambo unavyokuwa. Nilimsikia mmoja wao akisema: “Shia wana Qur'an nyingine ambayo imeongezwa na imepunguzwa.” Nikamuuliza “Iko wapi hiyo?”

Ulimwengu wa Kiislamu ulioenea kwenye mabara makuu matatu umedumu tangu kutimilizwa Mtume (s.a.w.) mpaka leo kwa karne kumi na nne haujui ila msahafu tu uliodhibitiwa mwanzo hadi mwisho, uliohisabiwa Sura, Aya na matamshi yake, ipo wapi hiyo Qur'an nyingine? Na kwa nini watu na majini hawaijui

nakala yake kwa muda wote huo mrefu? Kwa nini uzushi huu? Malipo ya aenezaye haya na kudanganya ili awafanye ndugu zake wafikiriwe vibaya basi yeye ndiye anayekidhania vibaya kitabu chao.

Msahafu huo huo mmoja unachapishwa Cairo, Mashia wa najaf (Iraq) au Tehran (Iran) wanautukuza na kupeana majumbani mwao bila ya kufikiria chochote ila kuueneza tu, kwa nini basi kuwazulia uongo watu na *wahyi* wa Mwenyezi Mungu?

Katika waongo hao hao kuna wasemao kuwa Mashia ni wafuasi wa Ali na Masunni ni wafuasi wa Mtume (s.a.w.), na kwamba Shia wanaona kuwa Ali ana haki ya ujumbe; huu wote ni upuuzi na uwongo mbaya sana.

Mashia wanaamini utume ujumbe wa Mtume (s.a.w.), na wanatambua utukufu wa Ali wa kumfuata Mtume (s.a.w.) na kushikamana na mwenendo wake, wao ni kama Waislamu wengine hawachukulii kama kuna kiumbe wa zamani au atakayekuja ambaye ni mtukufu zaidi kuliko Mtume (s.a.w.) ambaye ni mkweli na mwaminifu, na hakuna afaaye zaidi kufuatwa kuliko yeye kwa nini basi wasingiziwe uzushi huu?

Ukweli ni kwamba wale wanaogawanya umma baada ya kukosa sababu ya maana na kuugawanya umma ndipo wakategemea vijisababu hivyo.

Ndiyo, sikatai kwamba ziko tofauti za ki-fikhi na kinadhiria baina ya Shia na Sunni lakini tofauti hizi hazileti watu kutengana, hata kwenye madhehebu za Sunni zenyewe pia kuna hitilafu, bali hata ndani ya dhehebu moja pia (kati ya manne hayo).

Ni vizuri Shia watambue kwamba Sunni wanawapenda mno

Ahlul Bait na wanachukia sana wawachukiao. Na ni vizuri sana waelewe kwamba Shia wanashikamana sana na Mtume (s.a.w.) na wanachukulia kutofanya hivyo ni upotofu.

Ama tofauti za ki-fiqhi au ki-nadharia zina marejeo ya kielimu (mategemeo), nao nia yao ni nzuri katika Ijithad yao kama wata-pata, au kama watakosa pia watapata malipo.

Kuna watu watashikilia kusema, “Lakini huyo kweli amekosa” ndiyo, lakini kosa hilo lina uhusiano gani na nyoyo zenyenye imani?

Hebu tuseme hatibu amekosea irabu tu katika matamshi, au mwandishi kukosea imla, au mhasibu amekosa namba, au mwanahistoria kudhibiti tukio, yote hayo Je, kuna uhusiano gani wa makosa hayo na uhakika wa dini?

Ikiwa mtu anaamini, kama mimi, maana ya kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume (s.a.w.), na anaswali kila siku, ana-funga Ramadhani kila mwaka na anahiji, vipi mtawenza kumkufurisha kwa sababu amekosa katika baadhi ya mambo? Au iwe ni kweli pametokea makosa katika jambo hili au lile ambalo mimi silikubali, kwa nini tusitoe muda wa kutatua matatizo hayo badala ya vita vya mizozo au mapigano yatakayoondoa imani na kuipa nguvu sauti ya shetani?

Hitilafu za ki-fiqhi au kinadharia katika mambo mengi si mkate wa kula kila siku, na yanayotokea kwenye mizozo hiyo Waislamu wanaweza kuyatupa kando wakayasahau kisha wakajishughulisha na kujenga si kuvunja. Au kufanya kazi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu katika msikiti au katika nyanja zingine zenyenye faida.

Ama watu kujishughulisha na hitilafu ndogo au kubwa basi wajue katika dini hakuna hivyo udogo au wingi. Na wale wanaopupia kufanya hivyo basi kwa Mungu hawana kitu.

Anaendelea kusema **Sheikh Muhammad Al-Ghazali**: “Kila hitilafu zilizobaki kwenye zama zetu ni mwanya unaoleta madhara kati ya Sunni na Shia! Ni mwanya unaotumiwa na wakoloni kwa kuupanua zaidi ili uwe daima ni kitenganishi kati ya makundi mawili.”

MSHIKAMANO WA KIISLAMU

Sheikh mkuu wa chuo kikuu cha Al-Azhar cha Misri **ustadhi Mahmud Shaltut** anasema: “Hakuna ubaguzi katika Uislamu, wakati wa ubaguzi wa ki-jahiliya umepita, sisi sote ni Waislamu na madhehebu yetu yote yatokana na asili moja, nayo ni ujumbe wa Muhammad, Kitabu cha Mwenyezi Mungu (Qur'an) na Sunna za Mtume wake. Kwa hakika mimi na wanavyuoni wengi wa kishia tumeandikiana barua nyingi juu ya kupasa kuwe na uwéléwano na kuondosha kasumba iliyopo kati ya Sunni na Shia ambayo maadui na wakoloni wameitumia kuwatenganisha nchini Misri, Iran na Iraq.

Anaendelea **Sheikh Shaltut**: “Ukoloni unatafuta kutoboa tundu la umoja wa Kiislamu ili waurarue, kuutawanya, na kuleta chuki kati ya Waislamu, ambapo dini yao yawalingania kwenye neno la Mwenyezi Mungu: “**Wala msizozane msije mkafeli ...**”

Madhehebu ya Shia yana dalili zenyе nguvu katika masuala ya Waislamu na hasa yale yahusuyo hali zinazowahu watu (mambo ya maisha yao ya kila siku), na mtafiti mwenye kuzingatia hoja zao za nguvu zinazoshikamana na malengo ya sharia kati ka kutangamana jamii ataona”

Kisha Sheikh huyo mkuu akatangaza kukubali elimu ya Fiqhi ya Kiislamu isomeshwe katika Kitengo cha sheria (cha chuo kikuu) ya madhehebu yote yakiwamo ya Shia Imamiya na Zaidiya akasema:

“Nimekubalina na **Ustadhi Al-Baqouri** kwamba watu madhehebu washikamane na kamba ya Mwenyezi Mungu kuungana kwenye nguzo ya ujumbe wa Mtume (s.a.w.); naye waziri huyo ustadi **Al-Baqouri** amekubali mwito huo kwa vizuri sana.”

Katika mahojiano yaliyofanywa kati ya Ustadhi mkuu na gazeti la ‘*Al-Shaab*’ litokalo Cairo, alizungumzia kuhusu Shia na tofauti za kimadhehebu na akafafanua kwa kirefu nafasi ya chuo kikuu cha Azhar katika msimamo huo, kisha ufanuzi huo ulipelekwa kwa **Sheikh Shaltut** ili awatangazie Waislamu neno hilo la Uislamu, ndipo **Sheikh Shaltut** alizungumza nami akisema: “Uislamu umelingania umoja na ukafanya nguzo ya kushikamana kwa Waislamu ni kushikamana na kamba ya Mwenyezi Mungu na hiyo imetajwa katika Aya za Qur’an kama vile:

“Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyinyi nyote wala msifarikiane.” (Al-Imran).

Na kufarikiana kwa ujumla ni kufarikiana pia kwa sababu za kimadhehebu, ambapo madhehebu za ki-fiqhi za Kiislamu pamoa na wingi wake na kutofautiana njia zake, zote asili yake ni Qur’an na Suna za Mtume (s.a.w.).

Akazungumza athari za ‘*Ijtihad*’ katika hukumu, kisha nikamuuliza: “Sisi hatupingi *Ijtihad* lakini kilichotokea ni kwamba madhehebu yamefarikiana na kuwa mengi, je una rai gani juu ya *Ijtihad* pale ilipofikia katika kutofautiana madhehebu kulikojitokeza mionganoni mwa Waislamu?

Akijibu: “*ijthad* katika hukumu imekuwa ni uwanja mpana ambao madhehebu yanatofautiana kwayo, na licha ya kuwa mengi na kuhitilafiana kwenye hukumu nyingi na rai zao kuwa nyingi kwenye suala moja; licha ya hayo yote, wote wamekuwa wakiku-

tana kwenye msingi mmoja na neno la sawa la imani na kuki-tukuza kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake, ambaye amesema: **“Hadith ikiswihi basi ndiyo madhehebu yangu, na yapimeni maneno yangu kwa mapana ya ukuta.”**

Na hapa ndipo Shafi, Hanafi, Malik, Hanbali, (Suni) na Shia wali-posaidiana, na tofauti ya viongozi wa madhehebu zinadhishiri pale wanapoangalia njia hasa ya *Ijtihad* na wakaathirika na mapendekezo ndipo zikapatikana tundu zilitobolewa na adui wa daima, kisha akaendelea kuipanua tundu hiyo mpaka akaweza kupitia hapo na kuufikia umoja wa Kiislamu akaupanua, akawagawanya na kuwafanya wawe maadui, na athari yake ndipo wakashutumiana Waislamu wenyewe kwa wenyewe. Lakini wale walio nyuma yao wanawaita wakisema: “njooni kwenye neno la Mungu.”

Nikamuuliza Sheikh: “Je umezifuata rai katika Shia ambazo umeziona kwa kuwa zinafaa bila ya kuchukua rai zingine katika suala moja.”

Akajibu: “Siwezi kusahau nilipokuwa nikisoma ulinganishaji wa madhehebu kwenye kitivo cha sheria kwenye chuo kikuu cha Al-Azhar, nilikuwa nikiziweka rai nyingi kwenye suala moja (pamoja na rai za Shia) lakini aghalabu niliona za Shia zinafaa zaidi kwani nilikubali nguvu ya hoja zao. Vilevile sisahau nilikuwa nikifuata masuala mengi kwa madhehebu ya Shia na nikitoa ushahidi katika mambo yanayohitajiwa sana na watu kama vile uharamu kutokana na kunyonya au yale ya hali za kila siku zinazomhusu mwanadamu. Hebu tuone mifano ya masuala haya: Talaka tatu kwa tamko moja tu, ambayo hiyo hufanywa na madhehebu mengi ya Sunni kuwa ni tatu, lakini katika Shia huwa ni moja tu tena talaka-rejea, ndipo ikawa fatwa hapo haina uzani kwa mtazamo wa hukumu.

Kanuni zihuusuzo hali za maisha ya watu zaonelea kuwa kuna tala-ka inayofaa na isiyofaa kulingana na lengo la kukusudia kuacha au kuonya, lakini Shia wanaonelea kukusudia uwache hakuachi; nami napendelea rai hii.

Mtafiti hasa wa kweli ataona Shia mara nyingi dalili zao zina nguvu na zinaenda na malengo ya sheria za kutengeneza jamii.

Nikasema: “Je, Sheikh, waona tofauti zimeanza kuwadhiki Sunni na Shia?” Akajibu: “Wakati wa kasumba hiyo umepita na ukurasa wake umefungwa, na Waislamu wameshajua kuwa hitilafu za ndugu hazidumu, lazima ifike siku wahakikishe nasaha yao kwa baba yao, na moyo huu umeendelea kukua mpaka Mhanafi amemfuata Mshafi na Sunni kufuata Mshia na wakanufaika, maoni yakaungana hata tukafikia wakati wetu hivi sasa.”

Nilarudia kuuliza: “Je kuna hatua iliyochukuliwa katika kuvunja tofauti, na je mna ratiba gani hapo?

Ustadhi mkuu akajibu: “Nimeamua kwamba fiqh isomeshwe kati-ka Kitengo cha sheria ambapo mionganoni mwayo ni ya Shia Imamiya na Zaidiya.”

Vilevile Sheikh Shaltut amezumgumza na waziri wa wakfu **Ustadh Sheikh Hasan Al-Baqouri Al-Azhari** ambaye ni Msunni, kuhusu kasumba ya kimadhehebu baina ya Sunni na Shia na wajibu wake juu ya kupambana nayo na kuwa chini ya nguzo tukufu ya ujumbe wa Muhammad juu ya kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna, ndipo waziri alijibu kwa kutoa mwito kikachapishwa kitabu ‘*Al-Mukhtaswaru nnafi*’ cha Fiqh ya Shia na kikagawanywa bure.

Vilevile Umoja wa mlingamano wa madhehebu, ulichapisha

kitabu ‘*Majamaul- Ibayaan*’ kwa rai ya Sheikh wetu Abdul-Majid Salim aliyekuwa sheikh wa Azhar, nikaandika utangulizi wake, na pia kuchapishwa kitabu cha Imam wa Shia Abu Ali Al-Fadhil bin Hasan At-Tabrasi, mmoja katika wanavyuo wakubwa kwa Kishia.

Nikamhoji tena huyo Sheikh wa Azhar: “Je una uhusiano wowote kati yako na wanavyuoni wa Kishia?”

Alijibu: “Mimi na wanavyuoni wengi wa Shia tumeandikiana barua juu ya kuwa karibu, kuelewana na kuondoa kasumba zili-zopo kati ya pande hizi mbili zilizowekwa na wakoloni ili kuwat-tenganisha Waislamu nchini Misri, Iran na iraq.

Na katika mahojiano kati ya Sheikh wa Azhar **Mahmud Shaltut** na mwandishi wa gazeti la Kiran la ‘*Itilaat*’ mwandishi huyo asema: “Nilimuuliza Sheikh Mahmud **Shaltut** ujumbe wa Azhar hivi sasa ni upi” Akajibu: “Ratiba muhimu sana kwangu hivi sasa ni kupambana na kasumba hii ya kimadhehebu na elimu za dini kwenye anga ya udugu wa kutafuta ukweli kwa manufaa ya watu, Waislamu wakiweza kufikia lengo hili watakuwa na nguvu zenye mshikamano na watajiondolea mizigo iliyopita iliyowaleetae kasumba na kuwafanya duniani waonekane kama wanaofuata dini tofauti ambapo wao ni wa dini moja wanaoamini Mungu Mmoja, Mtume mmoja na kitabu Kimoja.

Nikamuuliza: “Lakini kawaida masomo yana tofauti za kifika nimeona kuna Mujtahid wengi katika historia ya elimu za Kiislamu na rai nyingi hata kwenye dhehebu moja.” Akajibu: Tofauti ya maoni ni dharura katika jamii, hilo huwezi kulikana, lakini kuna tofauti ya hitilafu za kasumba za madhehebu, na kuganda na fikra maalum tu hata kama fikra hiyo yaenda kinyume na dalili za mantiki. Kwa hiyo kuna tofauti na inawagawanya Waislamu, ama ya pili ni hitilafu ya insafu na utafiti ilio nyuma ya ukweli na kuheshimu kila kikundi rai ya kingine.

Maimamu wa zamani walihitilafiana kielimu lakini waliheshimiana, kushauriana na kubadilishana maoni, wakitembeleana na mmoja kuchukua elimu kutoka kwa mwingine.

Kwa hivyo sisi hatuini watu kwenye dhehebu moja, bali katika madhehebu ya Shia yaungane na ya Sunni, Waislamu wawe kwenye rangi moja ya kusaidiana na mapenzi, na waache usongo, kubandikana majina mabaya, na kudhaniana vibaya, Sunni anufaika na maoni ya nduguye Shia, na Shia kwa nduguye Sunni, maadam wote ni wa asili moja - Waislamu.

Wote ni umma mmoja na msingi mmoja wa walioafikiana tangu mwanzo wa historia ya Uislamu. Wana lengo moja la kuamrisha mema na kukataza maovu. Yaani, juu ya kutengeza imani na kufanya kazi pamoja wawe mmoja mmoja au makundi, wasisahau hilo wasiache masuala madogo madogo yawatenganishe.”

Nikamwambia: “Sheikh, Ndiyo, ni kweli kwamba Uislamu ni umma mmoja lakini je, ni nyenzo gani zitakazouhifadhi umoja huo?”

Akajibu: “Nyenzo ya kwanza ni ile iliyokuwa ya kuacha kasumba, kutafuta haki na kusaidiana, hili ni sharti la kwanza, mengine ni kama kufanya mafunzo ya Kiislamu kuwa mamoja, na kunaufaika na kila upande, vitabu vigawanywe, barua ziandikwe na vyuo vikuu na madrasa zijuane na kubadilishana wanafunzi na waalimu, au kushauriana, kutembeleana na kutafiti matatizo tofauti kama alivyosema Mtume kuwa Waislamu katika kupendana na kusikitikiana ni wamoja kama mwili mmoja, ambao kiungo kimoja kikiumwa basi mwili mzima utateseka kwa maumivu na homa.”

Nikamuliza: “Watu wanaelewa kuwa nyinyi ni viongozi wa mlingano wa umoja wa madhehebu, je nini hatua zenu juu ya umoja huo.”

Alijibu: "Jumuiya hii imeundwa mjini Cairo yapata miaka kumi iliyopita na aliyeisimamia kwa juhud kubwa ni ndugu yangu **Muhammad Taqi Al-Qummi** mwana chuoni Mshia wa ki-Irani."

Mwito huu niliupokea nikiwa kati ya roho mbili tofauti:

Ya kwanza: Ni wale wasiotaka uelewano na wanaoogopa fikra ambayo hawajaizoea, ikiwa baadhi ya wapinzani hao wanasema kuwa Jumuiya hii ni Sunni ya kuwafanya watu wawe Mashia, wengine wakasema ni ya Shia kuwafanya wawe Masunni.

Ama roho ya pili: Ni wale waumini walioshikamana na dini yao ambao hawaangalii dhahiri ya mambo tu, bali wanazingatia na kujua Historia ya Kiislamu mwanzo wake na ilipofikia, na wana-jua siri ya hivyo na hao ni wale wajuzi, wenye subira, na ndiyo kwa wao ikaanzishwa jumuiya hiyo nami niliipenda fikra hii tangu siku za mwanzo na niliupokea kutoka kwa **Sheikh Abdul Majid Salim** aliyekuwa Sheikh mkuu wa Azhar na nikajuwa kuwa **Sheikh Al-Maraghi** na **Sheikh Mustafa Abdul Razaaq** (masheikh wakuu wa zamani wa Azhar) wanaiangalia fikra hiyo kwa matarajio mema, ndipo nikalazimika nilitumie jarida lake la *Rasalatul-Islam* kwa kufanya utafiti wangu wa tafsiri ya Qur'an ambayo nimefuata utaratibu mpya katika kufafanua maelezo ya Qur'an, nikawa napokea barua nyingi kama zile za jarida hilo.

Katika maisha yangu yote nilizama katika kusoma Fiqhi kwenye utafiti huru ambao msingi wake ni dalili na hoja ili nitoe hazina, watu wanufaika na mimi nimeweza, na ndugu zangu wengi katika Jumuiya ya muungano wa madhehebu, walitaka nipayendelee maoni yasiyokuwa ya Sunni licha ya kuwa sisi ni Masunni, kwa ajili hiyo kanuni zinazohusu mambo ya watu za Misri hazikuchukua talaka n.k haya yote yatokana na madhehebu ya Shia. Na sasa naona ni wajibu wangu niingie Kitengo cha Sharia katika chuo kikuu Azhar nikitatifi fiqhi kwa njia isiyo na kasum-

ba ya kimadhehebu, lengo si jingine ila kufikia hukumu sahihi katika mambo yote ya Waislamu, na hasa ya ki-elimu. Imefikia mwanachuoni huyu mkubwa avae nguo yake imfaayo na watu wajue kuwa yeye ni mwanachuoni hasa na ni nguzo yao.

Na hapa ndipo Azhar itasimama msimamo adhimu juu ya Waislamu licha ya tofauti yao.”

Mwisho nilimuuliza Sheikh: “Nini mustakabali wa Kiislamu baada ya haya maendeleo ya kisayansi hivi leo?”

Alijibu: “Uislamu daima unakuwa kadri elimu inavyokuwa na kuendelea na kujua siri za viumbe na kufaidika na alivyopewa mwanadamu kuvitumia hivyo kwa sababu hii ndiyo njia pekee ya kumjua Mwenyezi Mungu na kuamini utukufu wake, dini ya Kiislamu inahimiza elimu kwani elimu ndiyo inayofunua ukuu wa ulmwengu huu jambo linalotia nguvu imani ya waumini juu ya utukufu wa Muumba wake. Mwenyezi Mungu amesema kweli! **“Wale walipewa ilimu ...”**

Amri za Qur'an na kutafiti ardhi na mbingu lengo kuu ni kutia imani nyoyoni mwa waumini.

Elimu ni njia ya kuhifadhi imani na kujikinga na unyonge, ndipo daima mimi hufurahi kila elimu inapokuwa, na nasaha yangu kwa ndugu na wanangu Waislamu wasishtushwe na vitisho vyta dhahiri na wasizubaishwe na vitu visivyo na roho kwa vyenye roho.

Naomba Mwenyezi Mungu awape Waislamu rehma kutoka Kwake, Yeye ndiye mwenye kusikiliza dua.”

**Muhammad Shaltut
Mwanachama wa wanavyuoni.
Wakuu wa mlingano wa madhehebu.**

Ustadhi mkuu amesema: “Moja katika mambo yanayokusudiwa na Kitengo cha Sharia ni mtaala wake mpya wa Fiqhi ya kulin-ganisha madhehebu za Kiislamu kwa misingi ifuatayo:

Masomo yawe ya madhehebu mbalimbali bila ya kuwepo tofauti ya Sunni na Shia. Yaani kwa namna hasa ya mtazamo na Ki-fiqhi, ki-hukmu na kidalili kwa madhehebu zote nne za Sunni maarufu na Shia ithnasheria na Zaidiya.

Hukumu inayoongoza dalili iangaliwe kuwafikiria na kutowafikiana na madhehebu ya mwalimu na mwanafunzi, ila faida kulinganisha ipatikane nayo ni kufafanua maoni yenye nguvu zaidi baina ya maoni mbalimbali na hapo kasumba itaondoka.

Na katika *Usuulul-Fiqh* pia, yaani kwa namna maalum ya kubain-ishaa maudhui za asili na hitilafu baina ya madhehebu manne ya Sunni na zitajwe sababu za hitilafu.

Na katika ilimu ya *Mustalah* ya Hadith na ya ‘*Rijaal* masomo yatakuwa ni yale waliyo kongamana Sunni na yale waliyokongamana Shia Imamiya na Zaidiya. Kama ambavyo masomo yatakusanya mapokezi mashuhuri na wenye *sanadi* ‘wa madhehebu zote mbili pamoja na kupanua utafiti huu katika masomo ya elimu ya juu ya Kitengo cha sheria.

Sheikh aliulizwa: “Kuna baadhi ya watu wanaonelea kuwa yapasa kwa Mwislamu ili ibada na muamala wake uwe sahihi, afuate moja ya madhehebu manne maarufu ambapo ya Shia hayamo je Sheikh, unakubaliana na Shia mathalan?”

Hapo Sheikh alijibu: “Uislamu hauwajibishi mtu kufuata madhe-hebu maalum unasema: Kila mtu ana haki ya kufuata madhehebu

yaliyopokewa sahihi katika hukmu na vitabu vyake na mtu anaweza kuhama kutoka katika moja ya madhehebu hayo na hapana makosa.

Madhehebu ya Shia Jaafariya, yajulikanayo kama Shia Ithnaasharia ni madhehebu kama zingune za ki-Sunni.¹

Yapasa Waislamu wajue hivyo, na waachane na kasumba bila ya haki ya kushika madhehebu maalum tu, dini ya Mwenyezi Mungu au Sharia yake haifuati dhehebu. Wote hao wanajitahidi na wanakubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu, yafaa kwa asiyefanya *Ijtihad* awafuate na kufanya yale waliyoyathibitisha kwenye Fiqh zao na hapana tofauti ya hilo katika ibada na muamala.

Sheikh Mahmud Shaltut pia ana utangulizi aliuandika kuhusu madhehebu yawe karibu, uliotolewa Cairo kwenye toleo la 55, hata **Sheikh Muhammad Al-Madani** ametaja katika kitabu chake '*da'watut-Taqrif*' mnamo mwaka 1966 A.D.

Sheikh anaeleza hatua zilizopitia juu ya mlingano na hata fatwa yake ya kufaa kufanya ibada kwa mujibu wa Shia Ithnaasheria. Huu hapa utangulizi wenywewe:

“Fikra ya kuwa na mlingano nimechukulia kuwa ni fikra ya msingi, na tangu siku ya kwanza nimejitolea kuisimamia, mionganii mwa yaliyofuatia ni Tafsiri ya Qur'an ambayo ilikuwa ikichapishwa kwenye jarida la '*Risalatul-Islam*' kiasi cha miaka kumi na minne mpaka ikatimu kitabu ambayo naamini ndiyo fikra yangu kuu na natarajia kupata thawabu za Mola wangu kwani analogeomea mja kwa Mola wake ni kufanya juhudini katika kutumikia kitabu cha Mwenyezi Mungu.

1. Ametaja Sheikh Mahmud Shaltut fatwa ya kufaa kuabudu kwa madhehebu ya Ki-Shia katika jarida la Risalatul Islam, Cairo, Toleo la tatu, mwaka 1959 A.D (1379 A.H).

Kwa njia hii nimepata kubaki kwenye ulimwengu wa Kiislamu kutokea nijue uhakika wa mambo mengi wasiwe na sauti moja. Na imenifanya nijue kuwa wengi wenye rai na fikra za Kiislamu, na nikaweza kutoa fatwa ya kufaa kuabudu kwa madhehebu ya Kiislamu yenyе misingi thabiti mionganı mwayo ni ya Shia Imamiya Ithnaashariya nayo ni fatwa iliyosajiliwa kutoka Jumuiya yetu na kueneza sehemu mbali za miji ya Kiislamu duni-ani, na wale wasio na kasumba macho yao yameburudika kwayo.

Nami naamini ni sahihi, na nayaunga mkono kila mara, kwa kuwaandikia wapendao na kuwajibu wapingao kwa nakala au redioni nikilingania umoja na kuzunguka kwenye misingi ya Waislamu na kusahau chuki mpaka ukawa ni ukweli uliothibiti unawapitia Waislamu kama jambo lao baada ya kuwa kwenye zama za unyonge wa kifikra, na mizozo ya kisiasa.

Hiyo Azhar nayo imeanza mwanzo wa kuwa karibu na wengine wa madhehebu mengine na kukubali isomeshwe Fiqhi ya madhehebu mengine, Sunni na Shia, masomo ya kihoga na kidalili bila ya kasumba ya mtu fulani, Vilevile nimejitelea kuunda jumuiya za utafiti za Kiislamu ambazo wanachama wake ni wawakilishi wa madhehebu tofauti.

Kwa hivyo ile fikra tunayoitumia na kuifanya bidii imejikita hivi sasa ikawa ni mahali penye utukufu.

Nilikuwa natamani, lau kama naweza nizungumze kwenye mikutano ambapo mu-Iraq akae na Mu-Iran, au Mlebanoni na Mu-Iraq au mfuasi wa Maliki akae pembeni mwa Mshia Imamiyya na Zaidiya pia waketi meza moja wakizungumza elimu, fasihi, tasawwuf na fiqhi huku kukiwa na roho ya udugu na mapenzi.

Nilikuwa natamani nitowe sauti kama ya mtu msafi wa moyo, mtaalamu, mwenye tabia nzuri ambaye mtu huyo ni Ustadhi

mkuu **sheikh Mustafa Abdul Razak**, au kama mtu muumin, mwenye nguvu, aliyejaa elimu ya madhehebu zote, ustadihi **Sheikh Abdul-Majid Salim**, au kama mtu aliye na uzoefu wa kutosha kama **Ustadh Muhammad Ali Aluba**.

Na pengine ningezungumza na wengi wengine kama hao kama vile Imam mkuu **Al-Haj Agha Husein Burujerdi** (Mungu amuweke pema) au Maimam wawili **Sheikh Muhammad Al-Husein Al-Kashful Ghita** na **Sayyid Abdul Mushin Sharafuddin Al-Musawi**.

Hao wameenda kwa Mola wao wakiwa radhi, wameridhiwa nasi, pia tuna ndugu walioamini fikra zao na wanaendelea kuziunga mkono, wao ni Maimam wa Kiislamu Mungu pia awape umri mrefu na azibe makosa yao kwenye njia ya haki.

Watu wenyе mawazo mafupi na wengine wenyе malengo mabaya walipiga vita hii, kwani kila umma haukosi watu kama hawa.

Hao ni wale wanaoziajiri kalamu zao kwa ajili ya siasa za mtafaruku, kupinga harakati zozote za utengenezaji na kusimama dhidi ya kazi yoyote ya kuwaunganisha Waislamu.

Nilikuwa natamani lau naweza kueleza yote kisha lifuatie jarida la *Rasalatu-Islam* ambalo limetekeleza amana yake likiwa la kupinga rai za wanavyuoni wa kila upande, ikawa ofisi ya Sunni inajifaharisha nalo kama vile Shia.

Nasi twamshukuru Mwenyezi Mungu kuwa fikra ya ulingano wa madhehebu imekuwa ni yenye kutajika kwenye Historia ya kutangaza Uislamu na imeleta athari kubwa.

Moja katika safari zangu za Cairo nilitembelea ofisi ya Darut-

Taqriib (Ofisi ya Ulingano wa madhehebu) kama kawaida nilipewa nakala ya kisa cha ulingano na fatwa ya ki-historia kuhusu madhehebu za Kiislamu, ambayo chini imetiwa saini na Ustadhi mkuu Sheikh Mahmud Shaltut nasi tumeitoa kopi yake kama ifuatavyo:

“Basi ni juu yetu sisi kwamba kufarikiana Waislamu kwa kila mmoja atetee rai yake katika kuteka na kila mmoja apambane fikra yake hii na mwendo wake ule; ni lazima tujue *kwamba* yote haya ni dalili ya kusihi si dalili ya kushindwa, na mapambano siku zote yanaonyesha mwamko si kifo.

Dini imeshatimiza pale ilipokamilika kushuka Qur'an. Uislamu wakati wa Mtume ulikuwa ni ulinganiaji na fikra.

Ofisi ya Sheikh Mkuu wa Chuo kikuu cha Al-Azhar.



Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu

Nakala ya fatwa aliyotoa bwana mkubwa na mwalimu mkubwa Sheikh Mahmud Shaltut, Sheikh (mkuu) wa chuo kikuu, kuhusu kufaa kufuata madhehebu ya Shia Imamiya.

Swali: Baadhi ya watu wanaonelea kuwa ni wajibu kwa Mwislamu, katika kutekeleza ibada zake na matumizi yake yote, afuate mojawapo ya madhehebu manne ndipo zitakapokuwa sahihi. Na katika madhehebu hayo manne, madhehebu ya Shia Ithnaashariya na Shia Zaidiya hayapo. Je, unakubaliana na rai hii na kukataza kwa mfano kufuatwa madhehebu ya Shia Imamiya Ithnaashariya?

Majibu:

Uislamu haukumlazimisha yeьте kufuata madhehebu fulani, bali tuseme kila Mwislamu anayo haki ya kufuata madhehebu yoyote katika yaliyonukuliwa kwa usahihi na yenye vitabu mahsus vya hukmu zake. Na mwenye kufuata madhehebu yoyote miongoni mwayo anawenza kuhamia kwenye madhehebu mengine, hakuna ubaya wowote wa hilo.

Madhehebu ya Ja'fariya yanayo julikana kwa jina maarufu la madhehebu ya Shia Imamiya Ithnaashariya inajuzu kuyafuatwa kama madhehebu mengine ya Kisunni.

Inatakikana kwa Waislamu walijue hilo na waachane na ubaguzi wa madhehebu na kung'ang'ania dhehebu fulani. Dini ya Mwenyezi Mungu na Sharia yake haifuati madhehebu fulani.

Mujtahid wote wanakubalika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Inafaa kwa asiyeweza kufanya utafiti na Ijtihad amfuate Mujtahid na kutumia kwa mujibu wa uthibitisho wa fiqhi yake, wala haku-na tofauti hilo kwa ibada au matumizi yote kwa ujumla.

Bwana mkubwa mwanachuoni mtukufu Ustadhi Muhammad Taqi Al-Qummiy katibu mkuu wa kamati ya kunganisha madhehebu ya Kiislamu.

As salamu alaykum wa rahamatullahi wabarakatuh

Baada ya salaam, ninafuraha kukuletea nakala yenyе fatwa niliy-oitoa ya kufaa kufuata madhehebu ya Shia Imamiya, nikitumai kuwa utaihifadhi katika mas-ala ya kamati ya kuunganisha mad-hehebu ya Kiislamu ambayo kwa pamoja tumefanya bidii kuianzisha.

Mwenyezi Mungu atupe Tawfiq ya kutekeleza ujumbe wa kamati hiyo.

Wassalaam.

Sheikh mkuu wa chuo cha Azhar.

Ikiwa Mtume aliweka dola yenyе misingi ya kuweka Sheria ya Qur'an, ilikuwa kwa hali yoyote ni dola ndogo kwa mipaka laki-ni yenyе nguvu, daima inayokuwa na kuzagaa, ikabaki tu ikamili-ke na kupanda utawala wake kwa misingi salama, ambayo ilikuwa ni mbegu ngumu mfano wa *Granite*, bendera yake ime-bebwa na watu waumini wacha Mungu wasioogopa mauti yatawafika wapi, kwani hiyo kwao ni sehemu ya maisha.

Wao hawakuogopa mtu wala chochote wala dola yoyote wala serikali, fikra zao ni kwenye usawa tu. Baadhi ya Waislamu

walioongozwa na Ali (a.s) walianza kujenga dola iliyoundwa na nadharia na fikra, kisha wakatofautiana maoni yao na wale ambao imani haijawaingia damuni.

Abdul-Hadi Musud Al-Ibyari.

**Mjumbe wa wizara ya elimu na mwongozo wa jamii
Cairo.**

MAHOJIANO

Baina ya mtunzi wa kitabu hiki na Ustadhi mkuu wa chuo kikuu cha Azhar.

Nilimuuliza Sheikh: “Aliyekutangulia marehemu Sheikh Mahmud Shaltut aliyekuwa Sheikh wa Azhar, alitoa fatwa ya kujuzu kufanya ibada kwa kufuata madhehebu ya Shia Imamiya, je nini maoni yako?”

Alijibu: “Mimi ni mionganoni mwa wanaopendezwa na Sheikh Shaltut kwa tabia, elimu, ujuzi wake mwingi wa kufahamu vizuri lugha ya kiarabu na tafsiri ya Qur'an na elimu yake ya usulul Fiqhi. Fatwa aliyoitoa bila shaka ni fatwa yenye misingi katika imani yangu. na kwa hakika tumeamrishwa tuwe na ulinganio kwa Aya: **“Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakane”**. Nami nahisi baada ya kuzuru miji mingi ya Kiislamu na kuchanganyika na wanavyuoni nimehisi kuna mapenzi mengi na kujuua siri nyingi za Kiislamu, na hamu yao kubwa ya kujuana na kuwa karibu na ndugu zao katika nchi nyingine za Kiislamu. Na tunataraji Mungu awawafikie Waislamu na aunganishe nyoyo zao, na katika kupendana huku ni kheri kubwa kwa Waislamu na hasa katika wakati huu ambapo Uislamu umeenea katika nchi ambazo hazizungumzi lugha ya kiarabu na hata viongozi wao kusilimu.”

Nikamuuliza: “Ukiwa kama Sheikh mkuu wa Azhar umeweza kuwa mwenyekiti wa mikutano mitatu ya wanavyuoni na ume-safiri nchi nyingi, je una maoni gani juu ya mlingano wa Kiislamu licha ya tofauti za madhehebu zao?”

Alijibu: “Katika hili hii yapasa Waislamu wasaidiane na watem-beleane, bali huu ni wajibu wa kwanza kwa Waislamu, na ilivyo ni kwamba Mwislamu ni kila yule apigaye shahada (*Ash-hadu an laa ila ill illah wa- ash-hadu anna Muhammadan Rasulu llah*) Uislamu haumtoki kwa sababu amefuata madhehebu fulani. Nimefaidika na kuwapa faida walio katika nchi za Kiislamu kwa ziara zangu huko katika kuandaa mkuruba huu, jambo hilo tunahimizwa na Mwenyezi Mungu: **“Enyi watu! Tumewaumba wanaume kwa wanawake na tukawafanya mataifa na makabilä mbali mbali ili mpate kujuana”** kujuana kumelinganiwa na Uislamu tangu zamani sana, kwani kujuana huleta kuzoweanwa ambako huleta mapenzi, nayo huleta kufahamiana huleta amani ambayo ni upendo na hili yapasa Waislamu wote walijue.

Miongoni mwa sheria za Kiislamu ni kwanza kutoa salam kwa maamkuzi ya Kiislamu ‘*Assalam Alaykum*’ hili mimi huliita ni neno la siri kati ya Waislamu. Mtu anapokuwa katika moja ya njia za jangwani, usiku au mchana kabla ya kusalimiana na mtu huwa na hofu ya aina fulani na shaka ya yule anayekutana naye, lakini asikiapo salaam hii basi hofu yake huondoka.

Hatusahau Hadith zinazolingania kupendana na kuhurumiana kati ya Waislamu kama: **“Hawezi kuamini mmoja wenu mpaka amempendelee nduguye lile analogipendelea mwenyewe.”**

Au: **“mfano wa waumini katika kupendana na kuhurumiana ni kama mwili mmoja, kiungo kimoja tu kikiuma basi mwili mzima utakesha na homa.”**

Jengine katika Uislamu ni kumkirimu mgeni, Mtume (s.a.w.) amesema: “**Anayemwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na amkirimu mgeni wake.**”

Nyingine: “**Jibril hakuacha kuniusia juu ya jirani mpaka nikadhani atamrithisha.**”

Nyingine: “**Mwenyezi Mungu amrehemu mtu mcha Mungu mkarimu anapouza, anaponunua na anapoamua**” Hadith kuhusu hili ni nyingi hazina idadi, lililo wajibu kwa Waislamu ni kutangamana na watu wengine wanaowapinga katika dini.”

Hapa, nilisimama nikamwomba ruhusa Sheikh nikaenda zangu.

Ifuatayo ni barua ya Ustadhi mkuu, iliyoadikwa mfungo pili mwaka 1397 A.H. aliyomwandikia Al-hajj Agha Hasan Said, mwanachuoni mkubwa wa kishia wa Iran, nami nainukuu:

Kwako Sheikh Hasan Said

Nimefurahi sana kuuzuru mtaa wa Ali bin Abi Talib, pamoja na rafiki yangu Talib Ar-Rifaai, ziara hii imenikumbusha ziara yangu niliyoifanya mjini Tehran mwaka 1970 A.D nikawajua wanavyuoni wengi wa kishia na nikajua ukarimu wao ambao sikujua hapo mwanzo. Na ziara yangu hii ya leo ni kuonyesha kutekeleza ukarimu wao, Mwenyezi Mungu awajaze kheri kwa bidii yao kuleta madhehebu zote karibu, ambalo hilo kwa kweli ni jambo moja katika misingi ya itikadi ya Kiislamu ambayo imewakusanya katika udugu kama ilivyosema Qur'an: “**Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu.**” Udugu huu ni wajibu kwa wanavyuoni wa Kislamu waupokee, licha ya tofauti za madhehebu zao.

Mungu amrehemu **Sheikh Shaltut** aliyezingatia maana hii tukufu akatoa fatwa yake wazi ya kishujaa alipozungumzia kuwa kufanya ibada kwa mujibu wa madhehebu ya Shia Imamiya (Ithnaaasheriya) kunajuzu, akizingatia kuwa ni madhehebu ya kifiqhi ya Kiislamu ya nyendo na Qur'an na Sunna. Namwomba Mungu awawafikie wale wanaofanya juhudi juu ya kuwaleta karibu wawe pamoja kwenye imani ya kweli ya Kiislamu.

Sheikh wa Azhar (wa zamani) Muh'd Al-Faham

12 Mfundo Pili 1397 A.H.

MAHOJIANO KATI YA MTUNZI NA MKUU WA MSIKITI WA CAIRO

Nilianza kwa kumuuliza mkuu huyo: “Nini maoni yako juu ya Shia, na jinsi mlango wa *Ijtihad* ulivyo wazi kwao?”

Alinijibu: “Fikra zao haziwezi kupuuzwa kwani wao wanawakilisha nusu ya Waislamu wa dunia nzima, hainiingii akilini *Ijtihad* yao ipuzwe au wafanyiwe uadui katika wakati ambao tunalingania umoja wa Waislamu chini ya ‘*Lailaha illa llah*’

Mashia wana *Ijtihad* nzuri katika fiqh sijui kwa nini Masunni wanawapuuza pamoja na kuwa wengi wao wanashirikiana na jamii yetu ya leo.”

Kama nilivyowaona huko Tanzania, Afrika ya Mashariki nilipokuwa nafanya kazi nikiwa mkuu wa kituo cha Kiislamu, niliona wanafanya kazi kubwa ya kuhudunia Uislamu katika eneo hilo, Vilevile nchini Kenya, Uganda, Zambia na Msumbiji, Vilevile wanasimamia kujenga na kuikarabati misikiti.

Nikamuuliza: “Vipi maoni yako juu ya fatwa aliyotoa ya kuabudu kwa mujibu wa madhehebu ya Shia?”

Akajibu: “Fatwa hiyo ya Sheikh ndiyo tunayoitumia hivi sasa, na Sheikh Shaltut ni Imam Mujtahid na maoni yake ni yenyewe kusibu, na ni jicho la haki, na kwa nini tugande kwenye madhehebu maalum tu na wote hao ni Mujtahid.”

Abdur-Rahman An-Najjar
Mkuu wa misikiti –Cairo.

MAHOJIANO NA USTADH ABDUL FATAH ABDUL MAQSUD.

“Ustadh nini maoni yako juu ya Shia na itikadi zao?”

Majibu: “Mimi kwa maoni yangu, Shia ni kioo safi cha Uislamu na atakaye kuuangalia Uislamu auangalie kupertia itikadi ya Shia na amali zao, na Historia ndio shahidi mzuri wa huduma zilizofanywa na Shia katika kulinda itikadi za Kiislamu. Na wanavyuoni wa Shia ndio waliofanya kazi kubwa ambayo hajafanywa na yejote, wamepigana na kujitoa mhanga kwa ajili ya kuinua neno la Mungu, kueneza mafunzo yake na kuamsha watu na kuwapeleka kwenye Qur'an.”

Kuhusu fatwa ya Sheikh Shaltut ya kufaa kufanya ibada kwa mujibu wa Shia.

Sheikh huyu alikuwa na haya ya kusema: “Sioni sababu ya madhehebu kuwa mengi ila ni njia tu ya kufafanua yale yaliyojificha katika hukumu za Kiislamu. Kutoka hapo ndipo madhehebu ya Shia yana haki kuwa kama madhehebu mengine, wala si makosa nikisema kwamba soma uchukuwe yaliyo bora kwa mwingine na hasa ukijua kuwa shina lake ni Imam Ali bin Abi Talib aliyekuwa mjuzi zaidi wa dini ya Kiislamu baada ya Mtume (s.a.w.).”

**BARUA YA SHEIKH AHMAD HASAN
AL-BAQIRI, WA WIZARA YA WAKF, ALIY-
OMWANDIKIA MTUNGAJI WA KITABU
HIKI.**

Ustadh Sayid Murtadha Ridhwani,

Assalam alaykum,

Nakushukuru kwa bidii yako kwa kutoa kitabu Wasailu Shia' ambacho twataraji kitafungua kurasa mpya katika kuwaleta karibu wafuasi wa madhehebu za Waislamu. Waislamu wali-farikana hapo zamani kwa sababu ya utengano kama huu uliokataa mawasiliano yao, wakadhaniana vibaya; na hakuna njia ya kujua kadhia ya hali hii ila kwa kufunua zile tofauti zilizoko kwenye makundi mbali mbali, tofauti za Sunni na Shia nyingi zinajitokeza kwa kutojua tu, kwani pande mbili hazikai kujifahamisha maoni yao na hoja wanazotofautiana..

Kuitangaza fiqhi ya Shia kwa Sunni, na kutangaza ya Sunni kwa Shia ndio njia yenyewe nguvu ya kuondoa tofauti baina yao.

Kwa hivyo kutoa kitabu kama hiki ni kazi inayostahiki shukrani kwa wenye kuisimamia.

Wassalam aleykum,

Wizara ya Wakf

15/2/1985.

HISTORIA YA KIISLAMU

Iko haja kwetu ya kuisoma historia kielimu na zaidi kuisoma kisiasa na kifiqhi kwa undani zaidi.

Haja yetu ni kubwa zaidi wakati tunapokubali kwa yakini kiasi ilivyofanya siasa ya Bani Umayya na Bani Abbas katika kuleta picha ya kimadhehebu na ki-fiqhi, na tunapojuja kwa yakini mate-so waliyopata Shia katika familia hizi mbili zilizotawala kwa muda wa karne nane kamili.

Haya wanayofanya wanavyuoni wa dhehebu la Shia katika kufafanua elimu ya Kiislamu nafikiri ni rududi ya mapinduzi ya kisaikolojia ambayo yamewasha moto siasa za Bani Umayya na Bani Abbas katika nafsi za Mashia, wafuasi wa Imam Ali na Maimam waliokuja baada yake.

Kukandamizwa kwa Mashia kulifanya imani yao ikawa imetulia nafsi mwao kiasi kwamba mapinduzi yao katika historia yamechanganyika na damu ya nyama zao mchanganyiko wa imani ya kweli katika nafsi za Waislamu. Shia kwa upande huu - kwa dhati - ni waumini .

Na imani hii yenye kina na mwendo huu unaofufuliwa na Shia katika kila karne hiyo pekee ni siri ya harakati hii katika ulinganiaji wao, nayo pia ni siri ya mwamko katika vitabu vyao, na hii ndiyo roho tuionayo vitabuni mwao.

Dkt. Hamid Hafna Daud

**Mkuu wa Kitengo cha Fasihi na Lughya ya Kiarabu
Chuo kikuu cha ‘Aynu Shams.’**

BAINA YA SHIA NA SUNNI

Namshukuru Mwenyezi Mungu Bwana wa viumbe vyote, rehma na amani zimfikie Mtume wa Mwenyezi Mungu, mbora wa viumbe, na juu ya Aali zake watukufu.

Siku nyingi zilizopita niliandika barua yangu iitwayo ‘Baina ya Shia na Sunni’ nikiwa na hamu Shia na Sunni wakutane katika kuanza udugu na mapenzi, na kung’oa kilichopandwa na maadui wa pande mbili hizo katika nafsi na kusababisha ugomvi.

Na nikataka kila kikundi kiangalie upande mwengine kwa jicho la mtu anayetafuta haki na kujua kwamba haki ndiyo yenyé haki zaidi ya kufuatwa.

Nikasema: “Itakapokuwa athari ambayo tumerithi kutoka kwa wazee wetu wema imetilia mkazo dharura ya kuipupia haki pale inapopatikana.

Na hekima ni kitu kilichompotea Mwislamu anapokipata popote pale hukichukua hata kutoka kwenye mdomo wa kaffiri, basi nase-ma wazi, mwenye akili haijui haki kwa watu bali huijua haki kwa dalili na hoja kwani akishajua ndiyo ashawajua watu wa haki.

Inakuwa muhimu kwetu sisi wa kizazi hiki tuipupie haki, tujihimize nafsi zetu kwayo na tuizungukie bila ya kumwangalia yule anayetuita kwayo.

Mwislamu ana dhamira ya kuheshimu kila mtafiti kwa kuangalia maoni ya wengine, hata kama watahitilafiana lakini wakati huo huo wawe marafiki vipenzi. Mungu amrehemu asemaye: “Tofauti ya imani haiharibu mapenzi.”

Uislamu umebeba bendera ya Uislamu ya juu pale uliposema:

“Lingania kwenye njia ya Mola wako kwa hikma na mawaidha mazuri.”

Yatosha fahari kwa Waislamu kuwa wao wamekutana katika misingi ya dini yao, hawakuhitilafiana kwayo; katika nafsi za Waislamu kumtukuza Mungu ni katika mambo matukufu.

Imani ya ufufuo, utume na kuwa Mtume wetu Muhammad bin Abdillah (s.a.w.) ni wa mwisho, na ukweli wa Qur'an na Hadith sahih kutoka kwake, wote hao Waislamu wanayatkuza kwa namna ambayo hapana dini yoyote inayotkuza kiasi hicho.

Mengi hayo nimeyasema katika ‘Baina ya Shia na Sunni’ japo sikusema yote kutokana na hali ilivyo.

Dkt. Suleiman Duniya.

Profesa wa Falsafa, Kitengo cha Usuulu dini

Chuo kikuu cha Azhar, Cairo, Na mkuu wa kituo cha Kiislamu New York.

WANAHISTORIA HAWANA USAWA KWA SHIA

Zimepita karne kumi na tatu katika historia ya Kiislamu, lakini ‘Insafu ya wanavyuoni’ wakati huo wanapotowa hukumu zao juu ya Shia zinakuwa na jazba na utashi zao, na njia hii ikiwa ndiyo sababu ya kuzusha rabsha hizi mionganini mwa makundi ya Kiislamu, na kuanzia hapo ndipo elimu ikapata hasara ya kukosa elimu za kundi hili na maoni ya watu wao.

Hasara ya elimu ikawa kubwa inapogusa Shia. Lau wanavyuoni hao wangeacha kasumba wanapoandika juu ya Shia au wajifunze kwa mbinu sahihi za utafiti, na wangetanguliza hukumu ya akili kabla ya hukumu ya moyo, na wangetanguliza maoni kabla ya mapenzi ya moyo, tungepata elimu nyingi kwa Shia na tungelin-ufaika sana na turathi za madhehebu haya.

Mtafiti muadilifu, anachukua kutoka kwa Shia kiasi kile ana-chochukua kutoka kwenye madhehebu mengine ya Kiislamu manne ya kiSunni.

Imam Jafar Sadiq aliyefariki mwaka 148 A.H ndiye aliyekuwa mwalimu wa Maimam wawili wa Kisunni: Imam Abu Hanifa Nuuman bin Thabit (aliyefariki mwaka wa 150 A.H.) ambaye kwa hilo Abu Hanif anakiri juu ya mwalimu wake akisema: “Lau si miaka miwili angaliangamia Nuuman” akikusudia miaka miwili aliyosoma kwa Imam Jafar bin Muhammad.

Imam Malik bin Anas naye anasema: “Sijaona aliye fakihi zaidi kuliko Jafar bin Muhammad.”

Balaa ilikuwa kubwa zaidi pale baadhi ya Muhadithina (wapokezi wa Hadith) walipojitokeza kwa watu, huku wamejitanda vazi la

elimu kutaka kujitkuza nafsi zao walipotangaza mapinduzi dhidi ya vikundi, na Shia ikawa ndio zaidi kwao, wakaharibu yaliyoandikwa na Shia, utafiti wa kielimu na kuwafungia milango ya ki-elimu.

Kwa bahati mbaya mwalimu wetu Ahmad Amin alikuwa mmoja wao ambaye alijinyima nuru ya maarifa kutoka nguzo kuu miongoni mwa nguzo za maendeleo ya Kiislamu nguzo ambayo Shia walitangulia wengine katika maendeleo ya kielimu, ukawa mwendoo huu uliosajiliwa na historia ya Kiislamu ni kama wa wengine waliofuta nyayo zake, katika waalimu wa vyuo vikuu ambaa walifadhilisha kasumba pofu dhidi ya fikra huru.

Hiyo si njia ya sawa inayofuatwa na watafiti wa hakika, na huenda likawa ndilo kosa kubwa zaidi la kihistoria lililowafunika watafiti hao na hawakuligundua.

Masingizio haya waliyowasingizia wanavyuoni wa Shia walipowabandikia kisa cha ‘Abdalla bin Saba’ na kudai kuwa kila uzushi au ngano zimeletwa na wanavyuoni wa Shia.

Wengi wanakosea wanaodai kwamba wanaweza kusimamisha Shia, imani yao na elimu zao hata wakielimika kiasi gani au hata wawe na uwaminifu ulioje katika kunukuu *nassi*.

Nasema haya kwa mkato, baada ya mimi mwenyewe kutumia wakati mwangi nikitatifi hasa imani za Shia Ithnaasheria, lakini sikupata cha maana kutohana na yaliyoandikwa na ulama wa Sunni.

Hamu yangu ya kuzidi kutafiti haikuzidi bali nilitengwa mbali na kutolewa kufikiria pale nilipotaka kufikia kwenye ukweli wake na hiyo ni kwa sababu ya utafiti butu nilioufanya kutumia vitabu vyaa uhasimu vinavyopinga madhehebu haya ambayo yanawakilisha nusu ya Waislamu duniani pote.

Kuanzia hapo nililazimika kuitafuta haki popote ilipo, na hima popote niipatapo ndipo nipime utafiti wangu wa kielimu kwa madhehebu ya Shia Ithnasherini na mengineyo.

Nako ni kuyasoma madhehebu haya kwenye vitabu vya wanavyuoni wa Kishia na nijue itikadi zao.

Ilivyo hasa ni kwamba mwenye madhehebu anayajua zaidi kuliko mhasimu wake hata mhasimu huyo awe hodari kiasi gani.

Isitoshe ‘amana ya elimu’ ambayo ni msingi wa mbinu za kisayansi ndiyo niliyouchagua na kuufanya kuwa ndiyo mtindo wangu wa kufanya utafiti na utunzi wangu, pale ninapotaka kugundua ukweli wa kiroho na kimaadili.

Amana hii iliyotajwa inataka uthabiti kamili wa *nassi* za Kishia bila ya kutegemea vitabu vya marejeo yao, kama si hivyo basi atakanganywa katika utafiti wake na utafiti wake hautakuwa na msingi thabiti.

Hilo ndilo lililonifanya nifanye utafiti wangu kwa kutumia vitabu vya Shia wenye nizijue itikadi zao nikinakili kwa mujibu wa walivyoandika wao wenye kwa mikono yao, na ndimi zao zilivyo tamka bila kupunguza wala kuzidisha, ili nisiingie kwenye kuchanganyikiwa kama wenzangu wengine.

Na yule mtafiti anayetaka kusoma ukweli wa wengine bila kuu-pata kwa wenye huyo anacheza, hana chochote katika elimu.

Ama wanavyuoni wa Shia wanajipa ruhusa ya kufanya *Ijtihad*, na wanafanya bidii sana na mlango wa *Ijtihad* haujafungiwa wanavyuoni wake katika karne yoyote mpaka leo hii.

Isitoshe, wao ni lazima kwao kuwe na Mujtahid wa zama zao na wanawajibisha wamfuate na siyo wamfuate aliyekufa, maadamu Mujtahid huyu ‘wa sasa’ anafuata katika *Ijtihad* yake- msingi na matawi- kutoka kwa waliomtangulia.

Hili siyo lengo langu ninaloliangalia kuhusu *Ijtihad*, bali jambo zuri katika suala hili ni kwamba Ijtihad hii tunayoisoma kutoka kwao inaenda na mwendo wa maisha na kukua kwake na inafanya nassi za kisharia ziwe hai na zenyе kuendelea kukua zinazoenda na wakati bila ya kubaki kwenye kuganda kukuwa elimu jambo tunalolishuhudia sana katika madhehebu ziwapingazo.

Ama picha ya pili ambayo watafiti wanaifungulia macho na kuwapeleka kuzama kwenye masuala yao kama vile mjadala wa wanavyuoni wa Shia au suala la ‘uzuri na ubaya’ wa mambo au jambo, au je jambo zuri ni zuri kwa maumbile yake au ni zuri kwa sababu Mwenyezi Mungu ameliarisha na kuwaamulia watu wake.

Na hivyo hivyo kuhusu jambo bayá je ni baya lenyewe au ubaya umekuja kwa kuharamishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ama sisi hatuoni cha kushtua au kukanganya, kwani Shia wamechukua hukumu za dini kwa njia ya akili kwa kadiri ya kuchukua kwa njia ya upokezi, na maoni yao juu ya wema na ubaya ni maoni ya Mu’tazila.

Kuna swalí moja limebaki tulijibu, kwa nini wameathiriwa na Mu’tazila au Mutazila wameathiriwa na Shia?

Watafiti wengi wanaona kwamba Shia wameathiriwa na Mu’tazila kwa kufuata njia ya kutumia akili, lakini mimi naweza kusema kuwa Mu’tazila ndio walioathirika na Shia na kwamba Ushia ni itikadi iliyotangulia ya Mu’tazila.

Mu'tazila ni mtoto aliyelelewa na Shia, na viongozi wa Shia walitangulia kuwapo kabla ya Mu'tazila.

Nakwambia hivi kwa kuwa tumekubali ukweli wa historia na hatuna shaka kwamba Shia walidhiiri tangu enzi ya makhalfa na kutokea kwa ukhalifa kwa Imam Ali (a.s) katika njia ambayo haina ubishi.

Imam Ali kabla hajafariki Shia walikuwa tayari ni kipote kinachotia changamoto vikundi vyote vyaa kisiasa na kidini katika Uislamu.

Kuanzia hapa naweza nikamfunulia msomaji mwenye kuzingatia kwamba Ushia, siyo kama wanavyodai watafiti wazushi, kuwa ni madhehebu yaliyonakiliwa tu au imejaa uzushi na mapokezi ya ki-Israeli au imetokea kwa Abdalla bin Saba na wengine watu wa kubuniwa tu katika Historia, bali Ushia, kwa mtazamo wa mbinu zetu za kitafiti za kisasa, ni kinyume na wanavyodai mahasimu wao.

Ni madhehebu ya kwanza ya Kiislamu yaliyojitalidi sana kwa mapokezi na kutumia akili.

Hebu nikupe picha ya tatu ambayo utaona kama inapingana na mbinu ya akili tuliyokuelezea hapo awali, nayo ni kufanya bidii sana kwa Mashia kuzuru makaburi ya Mawalii na Maimam wa Ahlul bait wa Mtume (s.a.w.), na kudumisha Swala tano, kuweka miadhara ya elimu na kuhuyisha kumbukumbu za Maimam wao kumi na wawili.

Ama Masunni wao wanakubaliana na ndugu zao wa Kishia Imamiya katika itikadi hii, kwani makundi mawili hayo yote yanaamini kwamba Mawalii na Maimamu na wote walio duniani

hawakunufaishi na lolote ila tu mpaka atakapotaka Mwenyezi Mungu likupate.

Vilevile hawakudhuru chochote mpaka atakapotaka Mwenyezi Mungu. Kwa msingi huu, sababu ya kuzuru makaburi ya watu hao ni kuiga yao mazuri na mazingatio na mawaidha katika kuadhimisha kumbukumbu zao, na hilo ni wazi kwa vikundi hivyo viwili.

Muungano huu umefika kilele cha muungano baina ya mataifa mawili katikati ya karne ya nne yakafikia mwisho wake shakhsiya ya Swahib bin Ubad ambaye aliongoza Mu'tazila na Shia katika nusu ya pili ya karne hiyo ambayo ilimu ya Kiislamu ilikuwa huko. Ukweli ni kwamba vikundi viwili Mu'tazila na Shia walio upande mmoja na Sunni na Masufi upande mwingine wote wana njia zao katika sifa za Mwenyezi Mungu.

Ama Masunni na Masufi wanapendelea kutetea ‘uhuru wa Mwenyezi Mungu’ yaani ana uhuru kabisa, kwa ushahidi wa Aya isemayo ‘**haulizwi alifanyalo**’ na kila upande una upande uupendao.

Ikiwa Mashia wanasema kama Imam Jafar Sadiq (a.s.) “Hapana kulazimishwa wala kuachiliwa jambo ni kati ya mawili’ wao hapo wanakubaliana kabisa na ndugu zao Sunni wanaosema kuwa mwanadamu ana sehemu ya hiyari (ana hiyari).

Dkt. Hamid Hafna

Mkuu wa kidato cha fasihi, Chuo kikuu cha Aynu Shamsi-Cairo.

SHIA NA FIQH YA KIISLAMU

Marejeo ya Fiqh ya Kiislamu yanatofautiana, na Shia wamekuwa na misingi yao hasa kutokana na tafsiri ya Maimam wao walivyokifasiri kitabu cha Mwenyezi Mungu na Hadith zili-zopokewa na wapokezi wao kwani wao ni wenye kuaminiwa, na Hadith za Maimam wao ni kama daraja ya *wahyi* kwa *isma* yao, hawafuati mbinu za Sunni wanazotumia za *istinbaat*, katika fiqhi ya Ahlul Bait kuna yanayotosheleza haja za anayetaka kufaidika. Na utapata ulamaa wao wanasibu katika mengi ya kuhukumu yanayonakili makusudio ya sheria hata kama hawazikubali kanuni za kufanya *istinbaat* kwa Masunni, mionganoni mwa tungo zao zinazofafanua hayo ni kitabu *Wasaailu Shia ila tahswili masaa ilu sharia* ambacho kimeandikwa na Hurrul-A'mily kimekusanya masuala mbalimbali ya fani hii na kitabu *Mustadirak al-Wasaail* cha Mirza Husein Nuri, hicho hukumu zake zinarejea zaidi kwenye misingi na kizuri kwa wanafunzi na watekelezaji.

Pamoja na hayo tofauti ya matawi si nyingi, mwenye kusoma kitabu *Al-iatisaa* cha Sayyid Murtadha atajua kuwa Sunni na Shia hawakutofautiana ila kidogo na hitilafu ya maoni ya wanavyuoni haifai kuwa ni sababu ya kuzuia ilimu ya siri ya *istinbaat*.

Na hiyo siyo yenye kuwatenganisha wanavyuoni. Masunni wana madhehebu mengi ya fiqhi lakini wanafaidika na fiqhi kwa kuan-galia vitabu vinavyohusu fiqhi ya kulinganisha.

Hakuna kinachodhuru dini kama kasumba, na baya zaidi kwa akili na watu ni kudhania vibaya na ubinagsi. Fiqh ya Kiislamu kwa Mukallaf wote ni moja, watu wa mijii mbali mbali wanaitumia kwa ibada kulingana na tofauti ya madhehebu.

Natamani lau Sunni na Shia wangebadilishana elimu walizo nazo iwe kama bahari inavyochanganyikana na kutoa Lulu na Marijani.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu akusanye neno letu na kutakasa nia zetu, ye ye ndiye Muweza wa ayatakayo. Rehma na amani zimshukie Muhammad na Aali zake na maswahaba –Amin.

Abdul Wahab Abdul –Latif

Mwalimu wa Kitengo cha sheria, Chuo cha Azhar, Cairo

15 Jamadal Akhra 1377 A.H - 5 Januari 1958 A.D.

HAPANA TOFAUTI KUBWA

Shia ni madhehebu ya Kiislam, kiibada na kimuamala haitofau-tiani na madhehebu manne ya ki-Sunni, na yanafanana sana na ya ki-Hanafi, Vilevile mtazamo wake wa kifalsafa unaenda sambamba na hisia zetu.

Wao katika Hadith za Ahlul Bait wana hoja zao za kifalsafa, wao wako nyuma ya Ali bin Abi Talib na wanasema kuwa ye ye ni khalifa naye ana haki zaidi.

Wameshikamana na haki hii na wakaitetea. Msimamo wa Shia unaonyesha jinsi nyoyo zilivyojengwa kwa imani zenye uhuru wa kimawazo na hilo ndilo liunalojulikana kwa ndugu zetu Shia kila mahali, nchini Iraq, Iran, Bahrain, Yemen, India, Pakistani na Brazil.

Watu wanapokosea ni kule kuitakidi kwamba Shia wako kwenye matukio na mizozo iliyanzishwa na Muawiya tu ... Hapana hii si kweli.

Watu walikuwa wafuasi wa Ali baada ya kufariki Mtume (s.a.w.).

Siku Maansari waliponadi ukhalifa na Muhajirin na Waarabu wengine pia waliponadi na hitilafu hazikwisha ila baada ya kukatwa na Umar.

Ama lau ingekuwa kwa Ahlul Bait peke yao pamoja na kuanzisha mashauriano na nasaha iliyokubaliwa na Uislamu, lau Umar angelitazama kwa mtazamo huu yasingetokea matatizo haya bali Uislamu ungelibaki juu milele na ukawa na nguvu zaidi, nasi huku Mashariki tungelikuwa na khilafa ya Kiislamu na dola ya Kiarabu inayolingana na Vatican ya Roma na nguvu za kimaada za ki-Maghribi

Haki husemwa, lakini ukweli wa mwanzo wa madhehebu ya Shia na falsafa yake haujulikani hata wanavyuoni wetu wa Ki-Sunni pia hawajui, jambo hilo ndilo lililosababisha chuo chetu cha Azhar kiweke mtaala hasa wa kusomesha madhehebu ya Shia na Falsafa yake katika vitengo vyake, tunatarajia hilo litafanya maoni yetu yawe mamoja, mizani ilingane na matarajio yetu yapatikane, Mungu ndiye mwenye kuongoza, mwenye utafiti.

Fikri Abu Nasr

**Mwalimu wa zamani wa fasihi ya ki-Arabu nchini Libya
Cairo.**

NI TAWI

Hapana shaka kwamba madhehebu ya Shia ni tawi muhimu kati-ka matawi ya madhehebu za Kiislamu ambayo yanafuatwa na watu zaidi ya mamilioni nchini India, Iran na Iraq.

Na ipo haja kwenye kila masomo yetu madhehehu haya yasomeshwe ili tuweze kufikia lengo letu ambalo ni kupata mwafaka baina ya madhehebu mbalimbali za Kiislamu zilizo ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu - Qur'an Tukufu.

Madhehebu haya yana misingi ya kifikra kama madhehebu mengine za Kiislamu na wanavyuoni wa Shia ni kama wa Sunni wanapata kila kitu kutoka kwenye mipaka ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na yana thamani kubwa katika medani ya Kiislamu, na katika kufufua turathi za dini wana sehemu kubwa.

Kwa kweli nimewaona wao ni wenyе harakati kubwa sana na maendeleo ya ki-elimu ya kipekee.

Ikiwa Shia wanaonelea kwamba Ali (a.s.) alikuwa na haki zaidi ya utawala kuliko Abubakr, Umar na Uthman, hilo siyo msingi wa dini, au si lenye kupinga chochote katika mambo yaliyotajwa na Qur'an au Hadith za Mtume (s.a.w.).

Haya ni masuala ya maoni tu katika utawala, ni masuala yanayohusika na nafsi ya mtu, na si aibu baadhi ya watu wakionelea kwamba kuna watu walio bora zaidi ya kushika nafasi hiyo kuliko hao walioshika hatamu ya uongozi, kuna wengi nimeona wanapinga Shia au masikilizano baina ya Sunni na Shia lakini wanaikimbia asili ya tatizo bila ya kuwa na sababu ya maana, mimi nionavyo haifai kuwa hivi.

Nimefuatilia kusoma vitabu vingi vya Shia na nimefuatilia maoni yanayosemekana kwamba yanahitilafiana na wanapoelekea Sunni nikagundua kuwa ni tofauti zisizo na msingi kwenye mizizi.

Tofauti kuhusu kumfadhilisha Ali (k.w.) ni tofauti ambayo si katika misingi ya dini, wala hawaivunji nguzo yoyote mionganoni mwa nguzo za dini.

Mtume (s.a.w.) alifariki dunia kama walivyofariki Makhalifa wane na maswahaba wengine. Wala hapana faida ya hitilafu katika kumrudisha mmoja wao au mwiningine katika utawala.

Lau tukifikiri kwamba Imam atadhiihiri siku zijazo basi ulimwengu wote utamngoja kwa sababu ye ye atatiwa nguvu na roho ya Mwenyezi Mungu.

Abdul Hadi Mas'uud Al-Ibyari

Mwakilishi wa wizara ya Elimu na mwongozo wa jamii –Cairo.

KUHUSU FIQH

Madhehebu ya Imam Jafar Sadiq (a.s) ni moja ya madhehebu ya ki-fiqh yaliyorithiwa; na Shia Imamiya wanarejea kwake kwa hukumu za madhehebu yao.

Madhehebu hayo yanategemea riwaya za Maimam kutoka kwa Mtume (s.a.w.), kutoka kwa wale waliopokea Hadith za Mtume wakafahamu maelekezo.

Shia wanakusanya Fiqhi moja, ya Maimam wao iliyochukuliwa kutoka kwenye Qur'an na Hadith. Hiyo inaitwa Fiqh ya Jafar kwa sababu Imam Jafar Sadiq ndiye aliyeikusanya kwa wingi na

kuieneza, na wanafunzi wake wamesajili asili ya Fiqh yake, kwa hivyo Mashia wanachukua kutoka kwa Jafar Sadiq.

Fiqh hii inaenda sambamba na madhehebu mengine manne kati-ka mambo mengi na inahitilafiana katika mambo machache tu.

Mfano wa tofauti hizo ni kama vile sharti kwa Shia kuwa na mashahidi wawili waadilifu wakati wa kutoa talaka, na haiwi bila ya wawili hao; hapa wanafuata kauli yake Mwenyezi Mungu **“Ishini na wanawake kwa wema na muachane kwa wema na washuhudie wenye uadilifu katika nyinyi.”** (Sura: 65-2)

Shia pia hawatotai talaka tatu kwa tamko moja tu au kwenye mahali pamoa, wala talaka ya kuapa kwao si talaka.

Mfano wa hitilafu zingine ni ndoa ya ‘*Mut’ā* ambayo Shia wanai-halisha na wengine wameiharamisha.

.”Wao wanategemea kauli ya Mwenyezi Mungu:

فَمَا أَسْتَمْتَعْتُمْ بِهِ مِنْهُنَّ فَأَتُوْهُنَّ أُجُورَهُنَّ فَرِيْضَةً
وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا تَرَصِّيْدَتِهِ مِنْ بَعْدِ الْفَرِيْضَةِ

“...Ambao mmestarehe nao katika wao, basi wapeni mahali yao yaliyo lazima wala si vibaya kwenu katika yale mliyokubaliana baada ya (kutoa) mahari ...” Sura 4-24

Ndoa hiyo ni mume kumwoa mwanamke asiyé na vizuizi vya kumuoa kisheria na lazima ipite ‘*iqdi*’ (kufunga ndoa), mahari, na urithi wa mtoto na ndoa iwe na muda maalum wa kwisha kwake.

Kwa ujumla Shia inahitilafiana na Sunni katika masuala ya

utawala (ukhalifa) na Uimamu, lakini Shia wanaafikiana na madhehebu manne ya Sunni katika misingi na matawi mengi ya dini na kuhitilafiana katika baadhi ya matawi ya dini.

Pindi tunaposoma kwa makini fiqhi ya madhehebu ya Shia tutayaona hayo, katika kuafikiana na ya Sunni, yatakuwa na utajiri mwingi usio na mfano katika kuwekwa sheria.

Fiqh hii na ufanuzi wa kuweka sheria haufananishwi na zingine hata za madola makubwa yenye maendeleo. Je wanaonaje sheria hii ya fiqh ya Kiislam ambayo yatokana na dini ya sawa kutoka Kitabu cha Mwenyezi Mungu kinachochukuliwa kuwa ni msingi wa kwanza wa kuwekwa sheria kwa Waislamu wote nayo kama alivyosema Mtume (s.a.w.): **“Ni kamba imara ya Mwenyezi Mungu, na ni njia iliyonyooka, mwenye kufanya kulingana nayo hulipwa thawabu, na aliyehukumu kwayo amefanya uadilifu, na mwenye kuilingania, amelingania kwenye njia iliyonyooka.”**

Na Hadith ya Mtume (s.a.w.) ndiyo chimbuko la pili katika machimbuko ya kuwekwa sheria ya fiqh kwa umma wote.

Neno alilosema au kitendo alichokitenda Mtume na kuthibitisha kwake jambo, ni Sunna ambayo lazima itekelezwe.

Shia wametia sharti kwamba Hadith ni lazima riwaya zake zipitie njia za Maimam wa Ahlul Bait kwa sababu nyingi:

1. Wao wanaamini kwamba Maimam ndio wajuao zaidi Hadith na siri za dini.
2. Wanaongozwa nao na kuwazingatia kuwa ni waongozi wa kwenye kheri, na njia ya sawa. Na hivyo ni vile ilivyothibiti ubora wao, na fahamu zao za hali ya juu kabisa.

Na kwa kuwa masuala ya Uimamu na ukhalifa ndiyo yanayoto-fautisha baina ya Sunni na Shia, ndipo masalata wakajaribu kuy-atenganisha kwa ajili ya malengo yao machafu.

Na ikiwa itawezekana basi ni muhimu kila taifa libihadhi hulka yake pamoja na kuchunga udugu wa Kiislamu na kuheshimiana. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awakusanye Waislamu kwenye neno la kheri.

Muhammad Abdul-Mun'im
Profesa wa Kitengo cha fasihi ya Kiarabu wa zamani Cairo.

ALI BIN ABI TALIB

Kuandika juu ya Imam Ali ni kuandika juu ya Imani na katika kivuli cha Imani, pia juu ya Uislamu sahihi na kuwatetea Waislamu wa zama zote waliokuwepo wakati wake na waliokuwepo baada yake, tangu uliposhuka ujumbe kwa Mtume Muhammad (s.a.w.).

Mimi nilikuwa nangoja nipate fursa ili niweze kuandika yanay-omuhusu mtu huyu mtukufu.

Kama ilivyotajwa katika kitabu *Al-Iswaab* alijulikana kwa ushujaa na kuwa mbele, basi je umashuhuri huu unaishia hapa tu?

Wapokezi wengi wamepokea kwamba: Ali bin Abi Talib ndiye kijana wa kwanza kuingia Uislamu, kwa maana ya kuwa hakushi kwenye mambo ya ujahiliya, basi je sifa hii itakuwa ni hii hii tu?

Ali ni binamu yake Mtume (s.a.w.) na alimchukua kuishi kwake kama mwanawe na alifunga naye udugu, kama walivyopokea wapokezi waaminifu wakimnukuu Mtume (s.a.w.) mwenyewe akimzungumzia binamu yake huyo.

Ali alikuwa daraja yake ni kama ya Harun kwa Musa (a.s) isipokuwa tu hakukuwa na Mtume baada ya Mtume Muhammad (s.a.w.).

Alikuwa ni waziri na Khalifa wake baada yake. Na *nassi* hizo ni hoja za nguvu kutoka kwa Mtume juu ya Uimam wa Ali. Je ishara hizi za wazi hazitoshi kuonyesha haki ya Uimam wa Ali?

Kuhusu suala la Uimamu, Ibn Masud amenena: “Tulikuwa tukimzungumzia mtu aliye mbora zaidi wa watu wa Madina ambaye ni Ali.

Bali hata Umar mwenyewe alikuwa akiomba kusiwe na tatizo ambalo Ali hayupo, alisema: “Lau si Ali angeliangamia Umar.”

Kuna upande ambao yapasa tuuweke wazi kwetu na kwa dunia nzima kwamba walimtenga Ali, vita vikauma baina ya Waislamu na kuishia kwa wenye nguvu kushinda na si wenye haki kushinda, kwani lau haki ingeshinda, angelishinda Ali; ushindi wake ulikuwa juu ya vitimbi vyaya wenye vitimbi na juu ya mali na silaha, utapeli na dhuluma.

Abdul-Hadi Mas’uud
Mwakilishi, wizara ya elimu na mwongozo wa jamii- Cairo.

SIFA ZAKE

Ali (a.s.) alikuwa yeye pekee ni umma, si kwa sababu alikuwa ni mlango wa elimu au wasii wa Mtume Muhammad (s.a.w.) au ushujaa wake kwenye kupigania haki au kufahamu kaida za dini hii, si kwa lolote bali ni kwa jinsi alivyochunga mambo ya Mwenyezi Mungu kwa maneno na vitendo vyake vyote hata aliweza kujidhiki nafsi yake kwa ajili ya maslahi ya Waislamu wote,

na kuwatanguliza wao na maslahi yao kabla yake ye ye japo hilo lilimtia dhiki nafsi yake.

Mathalani, wakati wa ukhalifa wake alikuwa mwadilifu katika hukumu na aliupa nyongo ulimwengu.

Wengine waliuendea mbio ukhalifa, lakini ukhalifa ulimwendea mbio ye ye na aliwatanguliza wengine kuliko maslahi yake na jamaa zake.

“Na wanatanguliza zaidi nafsi zao japo wao walikuwa na haja zaidi.”

Maswahaba waliokuwa mafukara aliwaweka sawa na kuwafanya kama roho yake au watoto wake.

Yeye alikataa kabisa kufanya jambo ila liwe lina maslahi kwa umma, alijichunga sana kufanya lolote kwa ajili ya maslahi ya kibinagsi.

Ibn Qutayba amepokea katika kitabu *Al-Imama was-Siyasa* kwamba Aqil bin Abi Talib alikwenda kwa ndugu yake Ali mjini Kufa (Iraq) akamwambia: “Karibu ... ni jambo gani lilokuleta ewe ndugu yangu?” Akajibu: “Mapato yangu yamechelewa, vitu vimepanda bei kwetu, na tumekuwa na madeni mengi, nimekuja kwako ili unisaidie.”

Ali akamwambia: “Wallah nilicho nacho ni changu tu.” Aqil akasema: “Watu wa Hijaz wanakujia kwa ajili uwape, nami utawapa nini? Na nitalipia nini madeni yangu?”

Imam Ali akamwambia: “Je, wajua kuwa mimi sina zaidi ya kidogo nilicho nacho? Au unataka Mwenyezi Mungu aniteketeze

kwenye moto wa Jahanamu kwa ajili ya kukupa wewe pesa za Waislamu?”

Na hapana shaka kwamba Aqil alikwenda kwa Muawiya ambaye hatofautishi kati ya halali na haram na anaichukulia hazina ya Waislamu na mali za Waislamu kuwa ni milki yake peke yake.

Hii ni picha ya wazi inayotuonyesha mfano wa Ali katika kuupa nyongo ulimwengu na kuweka mbele maslahi ya umma kuliko yake mwenyewe na watu na jamaa zake, nao ni mfano ambao haujaonekana kwa Swahaba yejote asiyekuwa yeye, kama ulivyo msemo wake aliokuwa akisema mara kwa mara: **“Ee dunia mhadae mwingine siyo mimi.”**

Nasema hivyo na nashuhudia kwake kila masuala mbali mbali aliyopelekewa ya kisiasa katika Uislamu. Umar alijitahidi katika ukhalifa akamvalisha Abu Bakr kishali chake akatoa hoja ya kufanya hivyo ni kwa ajili ya kuzuia fitna isitokee na hilo alikiri yeye mwenyewe mara nyingi.

Ama Ali yeye alisimamisha hoja kwa wazee hao wawili alipokuwa akienda kwenye kubwa zaidi kuliko hilo nalo la muhimu kufanywa kwanza baada ya kufariki Mtume nalo ni kumtayarisha kwa mazishi (yaani kumuosha kumkafini n.k) kabla ya mambo yote.

Abdulrahman bin Awf naye alijitahidi katika kuchagua mmoja kati ya watu wawili Ali na Uthman kwa ukhalifa nao ni katika wale sita walioleuliwa na Umar. Ali akamsomea *nassi* ya ahadi, Ali akakubali ahadi kiasi cha uwezo wake, Uthman naye akakubali *nassi* ya ahadi kile kiasi ambacho *nassi* yake ingekubali ili ukhalifa usiponyoke mikononi mwake.

Ali aliridhia nafsi yake kutokana na mkataba wa Bin Awf kwa sababu aliangalia maslahi ya Mwenyezi Mungu, Mtume na Waislamu kuliko cheo cha ukhalifa.

Ali alipata pale alipoiamsha jamii ya Kiislamu katika ubatilifu wa Muawiya aliywakosea jamii ya Kiislamu na kila aliyefuata mwendo wake. Hakuna aliyepigana akauawa akiwa upande wa jeshi la Ali (a.s.) akitetea misingi yake ila shahidi awe Mujtahid au mfuasi kwa sababu huyo Muawiya alikuwa katika kipote kiovu kilichomuua Ammar Yasir kama ilivyosema Hadith ya Mtume (s.a.w.)²

Nasema: Mfano wa Ali na hasimu wake ni kama watu wawili, mmoja ameinuliwa na roho yake kwenye neno la haki akachagua nuru dhidi ya giza, na mwengine akachagua vyta dunia akaanguka duniani akifunika na giza na malimwengu akabadilika kwa kubadilika hayo malimwengu, yakatokea naye umbali ulioje wa wawili hao! Hata hawawi sawa.

Dkt. Hamid Hafna Daud
Mkuu wa Kitengo cha fasihi ya Kiarabu
Chuo kikuu cha Aynu Shams, Misri.

BADO TUPO NA ALI

Enyi ndugu, utukufu wa mvua, utukufu wa haki, utukufu wa elimu nawasalimia kwa maamkuzi wa Kiislamu nikisema: *Assalam aleykum warahmatullah wa barakatu*, kisha nikiuliza nitumie lugha gani niweze kuwasiliana nanyi? Wengi wamenitan-gulia kwa tungo wakayachukua masikio yenu mpaka mmebaki hamna mahali, kisha najiuliza tena vipi nitaweza kuwashukuru na nimeshindwa kusema kuwa mimi nafaa kwa uwanja huo. Mimi

2. Mtume alisema kwamba Ammar atauwawa na kipote kiovu.

nasema kutokana na mengi waliyoyasema. Nasema kwa jinsi unavyonidhania vibaya, kwa jinsi munavyoniheshimu ndio nase-ma sawa lakini kama mmeona mniipe neno la hekima kwa hekima ya hali ya Imam Ali bin Abi Talib, utukufu wa Imam umenifuni-ka kiasi ambacho siwezi kukanusha.

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu nimeweza kuandika juu ya Imam Ali. Kwa fadhila zake Mwenyezi Mungu nimepata heshima hii nzuri, lakini kwa kweli siwezi kuwa nimeandika kitu hasa kuhusu Imam Ali. Imam ni mkuu zaidi kuliko kitabu hata kiwe kikubwa kiasi gani.

Imam ni mkubwa kuliko Mwanafasihi ye yeyote atakayemsifu hata awe ni bahari iliyojaa sidhani kama hili hamlijui, ikiwa nimeweza kuandika kitu ambacho mmeona kinastahiki heshima yake, basi nimeandika huku nikiwa na imani kamili na nilichokiandika; si kwa sababu Imam alikuwa shakhsiya kuu tu, au niwardhishe watu hawa au wale; bali ni kwa ajili nipate kijiridhisha nafsi yangu na dhamira yangu, mambo niliyoyaona kwa Imam sijayaona kwa mtu mwengine yeyote zaidi ya Mtume (s.a.w.).

Yeye alikuwa ni mkusanyiko wa sifa, kielezo cha hali ya juu cha nguvu, ushujaa na kupenda Uislamu.

Ndipo nilipompata Imam, nilijaribu kadri ya uwezo wangu mdogo, niandike kuhusu yeye nami, nataka kudhihirisha upande wake mmoja ulio muhimu kuliko Historia waijuayo watoto kwa watu wazima; nilitaka nionyeshe kuwa yeye ni mtu aliyejua kufu-ata Uislamu kwa usahihi, alifuata kila njia zilipopitia hatua za Mtume (s.a.w.).

Katika mwenendo wake alikuwa akiitafsiriri Qur'an kwa vitendo kwa mitindo wa maisha ya kila siku kwa watu wote.

Alikuwa hajali afuatwe na Mwislamu au mwingine la muhimu kwake ni kufafanua yaliyomo katika Qur'an yaliyojificha ambayo yataweza kuwaongoza watu wote kwenye kheri, uadilifu na haki. Enyi ndugu zangu, Imam ni *shakhsiya* ambayo haijawahi kuonekana ila kwa Mtume (s.a.w.) tu. Na hilo si ajabu; lakini je, Imam Ali ni nani?

Yeye ni binamu yake, ndugu yake aliyelelewa na Mtume (s.a.w.) aliyemuiza binti yake (Fatima) na ni baba wa wajukuu zake (Mtukufu Mtume).

Hakuna hata mmoja aliyepata daraja hii wala hakuna atakayefikiria. Mimi nilipoandika kuhusu Imam Ali sikudhani kama kutakuwa na yejote atakayeniambia neno baya.

Sikuandika ila kile ninachoitakidi kuwa ni cha kweli na kile ambacho nimekipata kwenye vitabu kuwa ni kweli.

Atakaposimama mtu na kunitaja kwa ubaya na aseme atakavyo, hiyo haina thamani yoyote maadam naamini kuwa ninachokiandika ni cha ukweli na nadhani ni cha ukweli na nadhani ni cha sawa kabisa.

Jana tu nilikuwa nazungumza, mara nikazungumzia juu ya baadhi ya Maswahaba. Maudhi yaliyonipata kwenye imani yangu ni kwa sababu niliwataja baadhi ya Maswahaba kwa uwazi, maneno ambayo waliyasema wao wenye, mimi sikuzidisha chochote zaidi ya waliyosema wao, waliokuwa wakati wao na waliyatenda kwa mikono yao pamoja na hayo kuna mtu alisema kwamba, katika kitabu changu kuhusu Ali nimezidisha. Ni Maswahaba gani hao ambao nimetia chumvi kuhusu habari zao? Muawiya? Amr bin Aas? Mughira bin Shuu'ba? Na wengine mfano wa wao?

Muawiya - kwa mfano yeye amebatilisha haki kuwa batili na batili kuwa haki na akataka kuvuta watu nyuma yake au baadhi ya watu wamsaidie katika batili yake.

Yeye alidai kuwa Imam Ali ndiye aliyemuwa Uthman, kisha hapo hapo akadai kuwa aliyechochea Uthman auawe ni Ali. Je hii ni sahihi? Ukweli amba Muawiya mwenyewe anajua ni kwamba Ali alikuwa ndiye mtetezi mkubwa wa uthman kisha Muawiya anajua kwamba yeye ndiye aliyetumia jeshi la watu wa Sham (Syria siku hizi) na akawaamuru wasimame tu nje ya mji na wasijiingize katika mzozo uliokuwepo, waangalie tu kitakachotokea kama mapinduzi ya Answari yakitokea basi ndipo wajitokeze, na kama Uthman atauwawa wasiingilie bali warudi zao.

Je yamkinika nimsifu Amr bin Al-Asi muuaji, au nichukue kauli ya mmoja wa wanawe aliposema ‘Ukitaka dunia uwe pamoja na Muawiya, na ukitaka Akhera uwe na Ali’ akachagua dunia akawa pamoja na Muawiya.

Je naweza kumsifu mtu kama huyu?

Je, nimsifu Mughira aliyekuwa wa mwanzo wa kuvunja haki ya Ahlil Bait ya ukhalifa? Au nintaje kama wanavyomtaja kuwa alikuwa tapeli? La bali nasema yeye alikuwa msaliti na khabithi!

Kama inavyojulikana kwenye baadhi ya vitabu kwamba, baada ya kufariki Mtume (s.a.w.) alipita Mughira bin Shuu’ba akampata Abu Bakr na Umar wameketi kwenye mlango wa Mtume (s.a.w.) akawauliza: “Mnangoja nini?” Wakajibu: “Tunamngoja huyu mtu atoke ndani ili tupate kumbai (kumuunga mkono) yaani Ali. Akakuenua mdomo kwa dhihaka: “Je mwangojea kubai mimba ya Bani Hashim? Akawageuza kule haki ilikokuwepo na kuwafanya wafuate upande mwininge.

Wote hao walitaka mimi niseme wao walikuwa ni watu watakatifu, wasiofanya ubatili, mimi siwezi kusema hivi katu.

Siwezi kusema sua halionekani, wakati linaonekana, siwezi kudai lisilo la haki. ikiwa watu hao (kina Mughira) wameitwa Maswahaba wa Mtume hii ni kinyume na ukweli.

Rafiki ni nani? Je ni yule rafiki mnayekutana kwa saa moja au masaa machache kisha kila mmoja akashika njia yake? Je rafiki yako ni yule anayekuwa jirani yako mwezi mmoja au mwaka au miaka miwili?

Je rafiki yako ni mnayepiga gumzo la muda mrefu au mfupi? Au ni yule mnayeishi naye pamoja kwa muda mrefu?

Kwa maoni yangu; rafiki yako ni yule anayekuhifadhi unapokuwa haupo na unapokuwepo anakuhifadhi kwa watu wako, mali zako, siri zako na kila kitu, ambaye anakuwa badili yako na kukutetea uwe uko au hauko.

Katika hao nani aliyemuhifadhi Mtume (s.a.w.)? Nani aliye mhidhia watoto wake na watu wake? Kwa kweli hakuna hata mmoja. Pamoja na hayo ewe ndugu yangu nisingependa kurefusha maneno kuwashambulia, ila tu labda niseme sisi hapa Misri twawapenda Ahlul Bait penzi ambalo naweza kulisifu kuwa ni penzi zito tuliloumbiwa nalo, hatujui vipi! Tumepata hasara damu zetu kwa vizazi hatujui kwa nini lakini tunawapenda. Katika sisi kuna wanaowakosea bila ya kukusudia, aidha kwa kutojua au kwa kufuata maoni ya Mustashrikina ambao wametuletea fikra za kugawanya Uislamu, nataraji nitaupokea udhuru huu wao.

Hebu wacha niseme kweli mimi, kama nilivyosema awali katika mkusanyiko huu, nashukuru kujaa kwa vitabu vy'a Sunni kwenye

maktaba za Shia na kutokuwa vitabu vya Kishia kwenye maktaba za Sunni.

Hii ni kweli sana lakini inabidi maktaba za Sunni zijae vitabu vya Kishia, mnadhani ni nani atakayesoma vitabu hivi vyenye utafiti wa ndani sana, isipokuwa mwanachuoni? Tena mtafiti anaetaka kufikia kwenye kulinganisha jambo moja na jingine.

Pamoja na heshima yangu kwa wanavyuoni wa pande mbili ila nasema hivi: Wanavyuoni sio kuwa wao ndio umma wote, wanaweza kuwa ni viongozi tu wa umma wa Kiislamu.

Ama madhehebu ya Sunni yalijimakini katika miji mingi ya Kiislamu ambapo Mashia walikuwa wakikandamizwa ila wachache hata jamaa zao Bani Abbas waliwatesa mno.

Kwa hivyo ninavyotaka ni wao Shia waandike vitabu kwa ajili ya Mwislamu wa kawaida ambao asilimia yao ni tisini na tisa.

Mkiwaandikia kitabu hao, kitabu chepesi tu ambacho rahisi kukifahamu ili ukweli wa Shia ujulikane hapo itawezekana maktaba zijae vitabu vya Shia.

Tuanze kuunda kizazi kipyta kijuacho ukweli wa Shia tangu wato-to wadogo na vijana, tuwatayarishie vitabu vyepesi vinavyooleza ukweli wa Shia.

Nyinyi mwajua kwamba Masuni wengi hawajui kila kitu kuhusu nyinyi bali wanatuhumu tuhuma ambazo hazihusiani na nyinyi.

Hata wanawatuhumu kwa ukafiri na kuwatoa kwenye Uislamu haya ndiyo yasemwayo, hata wanawatuhumu kwamba nyinyi mnasema: Utume uliteremka kwa Muhammad kimakosa badala ya Ali aliyekusudiwa, wanawatuhumu kuwa mnampanya Ali kuwa ni Mungu.

Haya nimeyasikia kwa watu ambao si wajinga bali ni wasomi. Kwa nini msingeeneza kuandika vitabu ambavyo vimemfundisha mtoto kuwa Uislamu ni mmoja ni Usunni au UShia?

Hili likitimia, niaminivyo mimi, itawezekana kujenga udugu wa Waislamu na kuzidisha ukaribu wao, na Uislamu utaweza kusimama kwa mara nyingine tena kwa miguu yake.³

MUSTASHRIKINA NA UKOLONI

Watafiti wengi wa Mashariki na Magharibu, wa zamani na wa sasa wamekosa katika kuelezea Shia kwa maneno ambayo hayana dalili wala hoja za kuaminika na hayo watu wanapokezana tu bila ya kujiuliza kama ni sahihi au ni makosa.

Miongoni mwa sababu zilizofanya wanafiki hao wasifanye uadilifu ni kutoangalia vitabu nya marejeo ya Shia, na wakitosheka na marejeo ya mahasimu wa Shia.

Hapana shaka kwamba mtafiti anayetaka ajuwe Historia ya Shia, itikadi yao au Fiqhi yao hapana budi ategemee mapokezi ya Shia kwenye upande huo.

Pia mionganoni mwa sababu za kukosekana (malezo ya) uadilifu kwa Shia ni ukoloni wa kimagharibi ndio uliotaka kupanua uhasimu kati ya Sunni na Shia na hivyo umma wa Kiislamu kupatwa na mgawanyiko, ndipo wale Mustashrikina wakaanzisha fani waliyoitiita utafiti huru wa kielimu.

Linalosikitisha zaidi ni kwamba baadhi ya watafiti wa Kiislamu wanafuata maoni ya Mustashrikina hao bila ya kujua ukweli wa makusudio yao.

3. Hotuba ya Ustadh Abdul Fatah Maksud aliyoitaoa katika hafla kubwa mjini Kharshahr -Iran, mwaka 1976 A.D (1396 A.H).

Shia ni jina ambalo tangu zamani linamaanisha yule anayemfuata Ali (a.s.) na anayeamini kuwa yeye ni Imam na kizazi chake (kile cha Maimam kumi na wawili) ambao hivi sasa wanaitwa Ithnaashariya.

Na ilivyo, Shia wanategemea kumfuata kwao Imam Ali, wakitoa ushahidi kutoka kwenye vitabu vyta Sunni. Na maafikiano kati ya Shia na Sunni katika misingi ya imani (kama Mungu Mmoja, Qibla, Swala, Saumu, Zakka, Hijja) yako wazi kabisa hawana tofauti juu ya hilo; tukitoa suala la Uimam tu kwani Masuni wanaona kuwa hilo si suala la Kiislamu la kuchaguliwa na watu, ambapo Shia wanaona ni suala la kimsingi na kwamba Imam aliyatajwa ni Ali (a.s.) na Uimam hautoki nje ya kizazi chake na ukitoka basi ni kwa dhuluma au taqiyya na Maimam wao ni kumi na wawili.

Na maafikiano ya fiqhi kati ya Sunni na Shia yako wazi kabisa ila kuna baaadhi ya tofauti za ki-matawi kama vile Ndoa ya muda (muta') ambayo imethibiti kuwa ilifuatwa kwa Masunni lakini haikufuatwa kwa Mashia.

Na maafikiano ya fiqhi kati ya Sunni na Shia katika misingi ya itikadi na hukumu za fiqh yako wazi pia ikiwa marejeo ya asili yao wanayoitegemea ni moja ambayo ni Qur'an na Hadith.

Upopo uliopo wa tofauti ya Sunni na Shia sio mkubwa sana kama vile ulivyo mathalani kati ya madhehebu ya Imam Malik na wafuasi wake na katika wapokezi wa Hadith, na Imam Abu Hanifa Nuuman na wafuasi wake katika watu wa rai.

Na tutapojua kuwa Sunni wanakubali ubora na elimu ya Ahlul Bait watoharifu, na kwamba wao wana daraja yao hasa ambayo hawalinganishwi na yejote na kwamba kuwapenda ni ukamilifu

.....

wa dini na hivyo ilivyotajwa kwa haki yao kutokana na ushahidi; tutajua kuwa tofauti kati ya Sunni na Shia haina hatari yoyote.

Katika vitabu vya Sunni kuna ushahidi wa kutosha wa elimu ya kipekee ya Imam Ali, Hebu tutoe mfano kidogo:

“Imepokewa kutoka kwa Umar (r.a) kwamba, alikwenda kwenye jiwe jeusi (*Hajarul –Aswad*), akalibusu kisha akasema, “Mimi nisingemuona Mtume (s.a.w.) akilibusu, basi nisingelibusu.”

Ali (a.s.) akasema: “Ewe Amirul Muuminina, jiwe hilo linadhuru na linanufaisha na hiyo ni ufanuzi wa neno la Mwenyezi Mungu aliposema:

“Walipokubali kwamba Yeye ni Mola Mtukufu na wao ni waja, aliandika mkatuba wao na kuuweka kwenye jiwe hili nalo litafufuliwa siku ya Kiyama likiwa na macho mawili, ndimi mbili na midomo miwili likimshuhudia aliyetekeleza ahadi, nalo ni lenye kuweka amana ya Mwenyezi Mungu katika kitabu hiki.”

Umar akasema: “Mwenyezi Mungu asiniache duniani ambapo wewe Abul Hasan haupo.”

Umar bin Al-Khattab, kama inavyoonyesha Hadith hii anabusu jiwe jeusi kwa kumfuata Mtume (s.a.w.) na hivyo ndivyo afanyakyo kila Mwislamu katika kumfuata Mtume (s.a.w.).

Ama Imam Ali, upande wa ilimu yake alijua kuwa jiwe hilo jeusi halidhuru wala halinufaishi, kama jiwe lakini alijua kuwa lau Mungu anataka lidhuru au linufaishe angefanya hivyo kwa kutaka yeye Mwenyezi Mungu, na hiyo ni kwa sababu ya siri ya ile ahadi ya zamani aliyochukua Mwenyezi Mungu kwa roho za

wanadamu katika ulimwengu wa tonoradi kabla ya kuletwa ulimwenguni. Nalo ndilo shahidi wa binadamu siku ya Kiyama.

Hapa mtu atapinga na kusema kwamba ‘Hili haliingii akilini’. Atajibiwa kwamba basi mambo mengi ya hukumu za kisheria hayaingii akilini kwa sababu yako juu zaidi ya utambuzi wa akili. Na dalili ya hilo ni ibada ya Hijja haitambuliwi na akili kwa nini mtu aanze kuzunguka jiwe jeusi lenyewe?

Kwa nini yakusanywe mawe Muzdalifa kwa kumpiga shetani? Kila jambo lina siri yake na kila mahali pana mambo yake maalum.

Kwa hivyo basi, kuna mambo kati ya itikadi ambayo alihusishwi nayo Imam Ali na dhuriya wake baada yake kuyajua, na hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye.

Kwa hivyo haifai Waislamu wasio Shia waghafilike na thamani ya turathi za Shia katika itikadi na fiqh. Na turathi hii imepokewa kutoka kwa Ahlul Bait, wao ni Maimam wa fiqh na ni mabwana wenye ubora wao na mahali pao kwenye nyoyo za Waislamu.

**Dkt Abul-Wafaa Al-Ghanimi Attaftazani
Mwalimu wa Kitengo cha falsafra ya Kiislamu, Azhar Cairo
6 Jamaad Than 1381 A.H.**

NIA YAO NI KUTIA SHAKA

Wale Mustashrikina wanaoangalia mambo kijuujuu tu, wameshindwa kuelewa msimamo wa Ali alivyopata katika *Ijtihad* pale wengine walipokosa ambapo hatuna haja ya kurefusha hapa, bali tumeandika kwa kirefu kwenye kitabu chetu kuvunja uzushi wa Mustashrikina.

Mustashrikina hao hawakujua kama Ali alitanguliza dini yake kabla ya dunia ya watu na ulinzi wa Mwenyezi Mungu zaidi ya kufurahisha watu.

Watu hao hawataelewa maana za ndani, kwa sababu siasa kwa mtazamo wao ni kuitumia fursa ya kutia shaka, kusema uongo, unafiki na kutokubali na kukubali mahali pa kupinga hayo mbele ya Imam mcha Mungu, kuna kitu kitukufu zaidi ya hicho amba-cho nguzo yake ni akili na msingi wake ni kudhihirisha haki na lengo lake ni maslahi ya watu wote.

Dkt. Hamid Hafna Daud

Mkuu wa Kitivo cha fasihi ya Kiarabu

Chuo kikuu cha Aynu Shams, Misri.

NDOA YA MUT'A KATIKA UISLAMU

Shia wanapohalalisha ndoa ya *Mut'a* wanategemea Aya tukufu isemayo:

“Na pia (mmeharamishiwa) wanawake wenye (wanaume zao) isipokuwa wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume. (Ndiyo) Shariya ya Mwenyezi Mungu juu yenu. Na mmehalalishwa (kuoa wanawake) minghairi ya hawa. Muwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila ya kufanya zina. Basi wale mnaowaoa mionganoni mwao wapeni mahari yao yaliyolazimishwa. Wala si vibaya kwenu katika (kutoa) yale mliyoridhiana badala ya yale yaliyotajwa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima.” (4:24)

Kigezo cha kupima Qur'an na lughya ya Ayah hii kiko wazi haki-na kificho wala fumbo, na lau tungetumia akili ambayo ni moja ya dini basi pia tusingeona kama kuna kasoro katika jambo hilo.

Kielimu, sioni kama kuna tofauti kubwa kati ya ndoa ya *Muta* ambayo ina muda maalum na ina uhuru wa kuongoza mpaka mwisho wa maisha yake.

Ndoa ya Sunni inadumu mpaka itakapokatika, na ndoa ya *Muta* pia inakatika mpaka ifungwe tena, hii ndiyo tofauti ya kivitendo kati yao.

Kile ambacho ni muhimu kukiandika ni kuwa pale ambapo Uislamu unalingania kwenye mashauriano na kuamiliana vizuri na kuondoa tofauti.

﴿ فِيمَا رَحْمَةٌ مِّنَ اللَّهِ لَمْتَ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَطَّا غَلِيظَ الْقُلُبِ
لَا نَفْضُوا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي آلَّامِرِ
إِذَا عَزَّمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ تَحْبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ ﴾

“Basi kwa sababu ya rehma itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao (Ewe Muhammad). Na kama ungelikuwa mkali na mwenye moyo mgumu bila shaka wangalikukimbia. Basi wasamehe wewe na uwaombee msamaha (kwa Mwenyezi Mungu) na ushauriane nao katika mambo. Na ufungapo nia mtegemee Mwenyezi Mungu (tu ufanye hili uliloazimia). Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao. (3:159).

﴿ وَالَّذِينَ آسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَمْرُهُمْ شُورَى بَيْنَهُمْ
وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴾

“Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri Zake) na wakasimamisha Swala, na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku. (42:38).

Katika wakati huu ambapo Uislamu unapigana na ubinafsi tunaona kuna wengine wanafahamu umadhehebu kimakosa na kama kwamba wapinzani wao si Waislamu. Sisi hatuko kwenye maoni haya bali kinyume chake kabisa kwani kutofautiana katika maoni ni njia ya kufikia kwenye kupata usahihi.

Na wakati ambapo Uislamu unatoa wito huo, utaona vikundi vinaleta tashwishi kwenye tofauti za kimadhehebu.

Ama sisi hatuoni kuwa matusi ni njia ya kukinaisha bali tunaona

ni njia ya kutengana na chuki, Mwenyezi Mungu asema:

“Tumewafanya makabila na mataifa ili mjuane”

Sisi tuonavyo hivi leo ni bora tusome masomo yenyе mwamko siyo yenyе kulala. Lengo katika dini yetu ni kufikia kwenye fahamu ya kweli kwa njia za elimu ya ndani si ya juu juu tu; na kwa njia ya mwamko wa jamii yetu kuelekea kwenye mahali panapolingana na dini hii thabiti.

Pengine njia hatari za tofauti zilizozungumzwa ni suala la *Mut'a* ambayo wanavyuoni wa Shia wamehalalisha na wa Sunni kui-haramisha.

Kabla sijajadili maudhui haya ningependa kutoa takwimu zili-zochapishwa na chuo cha Azhar na kugawanywa yapata miaka kumi na mitano, kama ifuatavyo:

Makosa ya jinai (ya ngono) yamefikia matukio 1359 mjini Cairo pekee (Gazeti la Al-Ihram 27, Februari, 1942 A.D).

Vijana 1,005 wamegunduliwa na magonjwa ya zinaa katika hoteli ya Cairo na watu sabini wameshikwa kwa kujihusisha na biashara ya kuuza wavulana, wakiiza wavulana kwa Pauni tatu (Gazeti la Al-Ihram 27, Desemba, 1941 A.D).

Katika ripoti za ofisi inayoangalia ustawi wa jamii wametoa taarifa ya mwezi wa Septemba mwaka 1941, Cairo kama ifuatavyo: Ofisi imewatia mbaroni chokoraa mia saba na kumi na tisa.

Wanawake tisini na wanne wameshikwa mionganoni mwao ni wasichana wanane chini ya umri mdogo.

Wanawake kumi na watano wamekamatwa katika danguro. Nyumba za kufikia wageni na mahoteli yafanyayo ukahaba.

Magawadi (kuwadi) thelathini na wanne wemeshikwa.

Watu kumi na watatu wameshikwa wakifanya ufula kwenye kumbi.

Ofisi imethibitisha kesi elfu moja na nne za ubakaji.

Kesi tatu za ununuzi wa vitabu vya ngono.

Hii basi ndio ripoti ya mwezi mmoja tu katika mji mkuu, je ripoti ya miezi na miaka ifuatayo itakuwaje? Na ripoti imejitokeza mara baada ya kuwapo ukahaba wa wazi.

Idadi ya watu waliopatwa na magonjwa ya zinaa katika majumba ya ufula ilifikia robo milioni mnamo mwaka 1931. Na hatusemi kuwa hii ndiyo baadhi tu, yaliyojificha ni mengi zaidi. Yanayotokea kati ya wavulana na wasichana kwenye mashule yako wazi. Na yanayaotokea ndani ya majumba kati ya marafiki na ndugu pia yako wazi. Na biashara ya utumwa mamboleo inafanya na vijana katika miaka wanayongoja kuoa, na hatukusudii uhuru wa biashara hiyo bali ule uhusiano wa mume na mke katika njia ambayo haiingii akilini, haikubaliki kidini na kimaadili.

Vilevile magazeti jinsi yanavyoandika juu ya matukio yanayokaririka hayahitaji kufafanuliwa, bali yanayotokea mashambani yanashinda yote hayo.

Qur'an ilishuka ili kutengeneza na kulinda jamii, ilishuka kwa ajili ya watu wote licha ya hali na tofauti zao.

Ndoa imewekwa kwa ajili ya kuhofia zinaa, lakini hiyo ni ndoa salama kwa mke na mume bila ya kuathiri mwenendo wa mwanadamu au kuporomoka familia na ufumbuzi sio kuzini, ulawiti au kusagana. Maradhi haya yamejitokeza kwa sababu sisi hatukufahamu katika Qur'an kigezo tunachokitafuta katika 'tasawufi' au tukio tunalolitafuta katika Aya isemayo:

"Mmeumbiwa kutoka nafsini mwenu wake, ili"

Kwa matukio haya na tabia ya mwanadamu ya tamaa ilivyo ndipo akaruhusiwa aoe wawili au watatu au wane bali pia Mwislamu amefunguliwa mlango mwingine, nao ni ruhusa aliyopewa katika kauli yake Mwenyezi Mungu.

Wanajaribu baadhi ya Masunni kusema kwamba *Mut'a* hapa ni ile ndoa ya kudumu ya kawaida, lakini madai haya hayakubaliki kwa sababu istilahi ya *Mut'a* yajulikana; na ilikuwa halali wakati wa Mtume (s.a.w.) na wakati wa Abu Bakr na kipindi kidogo wakati wa Umar, na kwa Shia hiyo ni halali mpaka leo.

Vilevile kuna wanavyuoni wa Sunni wanaifasiri wakati mwingine kwa maana ya 'chenye kumiliki mikono' hii ni kujaribu tu kuhepa ukweli, 'kinachomiliki mikono 'hakihitaji ufanuzi na wala siyo makusudio ya Aya hii.

Hii ndiyo tafsiri walijotufafanulia Maimamu Mujtahidina wa Shia. Ama wote walijikalifisha kutoa wajihii usio huu wao ni wenyewe kuharamisha kile alichokihalalisha Mwenyezi Mungu na vile nionavyo hayo ni maelezo yasiyo na njia.

Tumeona tuchague maelezo ya Imam Ibn Hazmi, katika mlango wa 'Nikah' kuhusu *Mut'a*. Nasi twaongeza, baada ya utafiti huu mrefu kwamba wengi katika wanavyuoni wa Sunni na Shia

wamesema kwamba ndoa iliyotajwa katika Aya hiyo tukufu inazungumzia ndoa yenyeye muda maalum, nayo ndiyo marejeo ya mwanzo ya uhalali wake.

Ama kufutwa *Mut'a* wanavyuoni wa Sunni wanasema huko kumejua kutokana na Hadith ya Mtume (s.a.w.), lakini sisi tumezoea kwa Qur'an Tukufu inapoharamisha kitu huwa inakifafanua, kukikariri na kukisisitiza bali hata pia huwa ni dhambi kwa waki-tendao.

Mwenyezi Mungu amesema: “**Mwenyezi Mungu amefafanua aliywaharamishia.**”

Ikiwa *Mut'a* imehalalishwa kwa kutajwa na Qur'an Tukufu basi hapana budi iharamishwe kwa njia hiyo hiyo kwa kuifafanua.

Huenda mtu atasema kwamba kufungua mlango wa ndoa ya muda kutafunga mlango wa ndoa ya kudumu, lakini hoja siyo ya nguvu, haina haja ya kuijadili, kwani, licha ya kuhalalishwa *Mut'a* katika nchi kama Iran, Iraq na zinginezo bado ndoa za kudumu ndizo nyingi.

Au tuseme: Licha ya kuwa halali talaka kwa Masuni na Mashia kwa usawa hapo kila mwenye kuoa hataki kuitumia ruhusa hii ya halali kwa ajili ya kuhifadhi watoto, na hapendi talaka ila mtu asiyejua au asiyeweza kubeba jukumu au kutokana na dharura ya jambo ambalo sheria imeruhusu kwa ajili yake.

Mara ngapi wake wamewaudhi waume zao kwa haki au bila haki, bali aghalabu wamewadhuru miili ya waume zao lakini pamoja na hayo waume wakaonelea ni bora wahifadhi ndoa au watoto wake wa kiume au wa kike.

Ama *Mut'a* kwa Mashia inaondoa maovu mengi yanayotisha kuangamiza jamii, tumeona takwimu inayoonyesha maovu hayo, akiwamo mume na mke, akiwamo jirani aliye karibu anayejificha chini ya kivuli cha ukaribu wake, na licha ya makosa haya yanayojulikana na watu wote bali wanayoyaona hata kwa watoto wao bado wanavifukia vichwa vyao chini ya mchanga, na hii haiondoshi matatizo ya jamii.

Bali *Mut'a* inaondoa ufuksa ulio rasmi na usio rasmi. Na pia inashinda mzinifu anayetembea kama mnyama mara kwa huyu mara kwa yule, au Malaya anayejipeleka kwa huyu na kwa yule bila ndoa na ushahidi au kuzingatia eda ambayo katika *Mut'a* ya halali kwa Mashia ni kupita hedhi mbili kamili au siku arubaini na tano kamili ili kwamba lau itatokea mimba basi katika muda huo babake atajulikana, na atakuwa ni mwenye kubebe jukumu la mtoto huyo, jambo linaloweza kusababisha uhusiano wa ndoa ya kudumu.

Ama Uislamu umekuja kupigana na maovu yote haya na si kupigana kwa upanga kwani huo ni dhaifu sana katika kutatua matatizo, upanga unapompiga mwizi unasahau kwamba rushwa ni mbaya zaidi katika kuvunja umma kuliko wizi. Upanga unapopiga umalaya bila ya kupanga mbinu za kurahisisha ndoa, unasahau kwamba hulka ya mwanadamu ina nguvu zaidi kuliko maji, mawimbi yenye nguvu na mioto mikali.

Msingi wa Uislamu ni imani kwanza kabla ya upanga. Hii ni fikra yenye nguvu ambayo sisi twaamini kwamba ina nguvu zaidi kuliko majeshi ya duniani. nayo ndiyo msingi wa kuunda jamii katika nguzo yoyote mionganoni mwa nguzo za duniani. Na msingi huo fikra yake ya kimaendeleo inaenda na tabia za mwanadamu. Mwisho tunaonyesha tofauti baina ya ndoa ya *Mut'a* na ndoa inayofanywa na Sunni:

Ndoa ya *Mut'a* ina muda maalum na anayeifanya ana uhuru wa kuiongeza mpaka mwisho wa umri. Na ndoa ya Masunni – ile ambayo haina muda maalum – yule anayefunga ndoa hiyo, kwa maelezo ya Qur'an Tukufu, anaweza kuikatiza kwa talaka.

Kwa hivyo basi, ndoa ya halali kwa Masunni ni yenyе kudumu mpaka pale inapokatika; na ndoa ya *Mut'a* ni yenyе kukatika mpaka inapounganishwa, hii ndio tofauti baina yao.

Tofauti hii hatuijali sana mwisho tunasema kwamba dini hii ni thabiti na yapasa wanavyuoni wazame kwa upole na pia yapasa wachunguze matatizo yake kwa utafiti huru usio na kakamio, na kisha utafiti wao uonyeshwe watu kwa njia zake kwa namna ambayo hakutakuwa na tofauti baina ya Waislamu itakavyoleta madhara.

Abdul –Hadi Masud Al-Ibari.

**Mwakilishi wa Wizara ya Elimu na Mwongozo wa jamii,
Cairo.**

MASWAHABA WA MTUME (S.A.W)

Kitabu kilicho cha ukweli zaidi ni Qur'an, bora ya uongofu, ni uongozi wa Mtume Muhammad (s.a.w.), ubaya wa mambo ni uzushi, na kila uzushi, ni bid'a na kila bid'a ni upotevu na kila upotevu ni motoni.

Abdalla bin Masud alikuwa akifungua darsa zake kwa Maswahaba wenzake na wanafunzi wake kwa maneno haya na anapoanza kuzungumzia elimu alikusudia ni yale yaliyo matukufu zaidi wanayokusudia wanavyouoni wa dini na watafutaji ukweli kwa kwenda nyuma ya haki pekee na kujiepusha na upotofu na ufidhuli, na hakuna njia ya kulifikia hilo ila kwa kushikamana na nguzo mbili za dini ya Kiislamu ambazo ni: maneno ya Mwenyezi Mungu na ya Mtume wake (s.a.w.).

Ama nguzo ya kwanza ni haki ambayo haiingiliwi na ubatili mbele yake wala nyuma yake, imeshuka kutoka kwa Mwenye hekima Mwenye kushukuriwa nayo ni maneno ya Mwenyezi Mungu mtukufu, muujiza kwa watu, inayotoa dalili ya utume wa Muhammad (s.a.w.).

Ama nguzo ya pili: “Na kwa kuwa maneno ya Mtume huyu mwaminifu mwenye kutamka kitabu cha Mwenyezi Mungu yeye hatamki kwa utashi wake bali kwa *wahyi*, na hasemi ila ukweli ambaao ni *wahyi* kutoka kwa alikofundishwa na Mwenye Nguvu (Allah). Mwenyezi Mungu amemsifu Mtume (s.a.w.) katika Qur'an:

“Na kwa hakika wewe u mwenye tabia tukufu kabisa.”

Kwa hivyo, kila kinachokuja kwa kutumia njia mbili hizi, basi ni kweli iliyo wazi ambayo haina ushindani wala shaka, na kila kina-

chokuja pasipo njia hizi mbili hicho chawenza kukosolewa, kunyoooshwa, kutengenezwa na kurekebishwa.

Nadhani msomaji makini ameelewa ninayoyakusudia kwa kusema hivi, yaani, maneno haya yenye hekima aliyokuwa akiyatuma swahaba huyu kufungulia darsa zake, alikuwa akikusudia jambo kubwa katika upande wa ‘kuweka Sharia ya Kiislamu’ nako ni kutegemea Qur'an na Sunna.

Ama Qur'an iko wazi na maneno yake yanakubaliana na hayana ushindani wowote.

Mara ngapi Mtume amewasifu kundi la Maswahaba waliokuwa wanyonge mno na maskini sana lakini walitukuka kwa imani zao, wakifiki mawinguni kwa fadhila za ikhlasi zao katika mwito wa dini na kumpenda Mtume na Ahli (jamaa) zake baada yake. Miongoni mwa wanyonge hao ni: Salman, Ammar, Abu Dharr na Miqdadi.

Lau ubora huu ungelikuwa kwa misingi ya ukubwa wa nasaha na utukufu wa kabila na utajiri na uzuri, Mtume asingelisema kuhusu Salman Al-Farsi: “Salman ni katika sisi Ahlul Bait.” Hiyo ni kwa sababu nasaba ya ucha Mungu na daraja ya imani inakata zote na inapanda juu kwenye heshima.

Hivi ndivyo Mtume alivyoono vizuizi vyta utabaka (ya wengine kuwa mabwana na wengine watwana) aliondoa ubaguzi huo hata kabla wanafalsafa wa siasa ya ujamaa hawaajaleta fikra hiyo miaka mingi iliopita.

Na hivi ndivyo alivyokuwa akimnusuru mnyonge mcha Mungu juu ya mwenye nguvu, mwovu, wakati alipowawekea watu mizani ya uadilifu na kuwafanya wote wawe sawa mbele ya mizani hii.

Maelezo yamekuja juu katika Qur'an, Hadithul-Qudsi na katika Hadith za Mtume. Je, baada ya hayo watu watafute desturi gani kubwa ya kuitegemea iliyo kubwa ya kufaa kuwakosoa Maswahaba? Maswahaba, na watu wote, kwa mtazamo wa dini hii wanashindana ubora kwa ucha Mungu na kwa kiasi cha taufiq walioipata katika kufuata misingi hii.

Swahaba, uswahaba wake hauwafiki ikiwa hakushikamana na aliyokuja nayo Muhammad (s.a.w.) ikiwa wamefahamu misingi hii na wakashikamana nayo sawa sawa.

Mara ngapi mtu aliye karibu ni kama wa mbali, na wa mbali tu karibu? Nasema hivi: Sisi na Maswahaba, katika kulingania haki na kufikisha ujumbe aliokuja nao Mtume kwa watu, tuko sawa sawa. Ndiyo heshima kubwa yao ni kule kumwona Mtume na kupokea kutoka kwake, lakini lazima tujue uswahaba huu una njia mbili zinazojitokeza, nazo ni neema kubwa na hoja yenyе nguvu.

Na nakusudia kwamba, lau huu uswahaba ungeweza kumwombea swahaba au kumkinga asikosolewe au asipatwe na mtihani, basi Mtume asingelisema kumwambia mwanawewe (pande la nyama yake tukufu na bibi wa wanawake duniani) "Ewe Fatima bint wa Mtume niombe utakacho, mimi sikutoshalezei chochote kwa Mwenyezi Mungu" Maneno hayo aliyasema pale iliposhuka Aya: "**Na uwaonye jamaa zako walio karibu.**"

Ndiyo, misingi ya kielelezo cha uadilifu aliyokuja nayo Mtume inaweka watu wote sawa mahali pamoja, wakati wa kutekeleza hukmu.

**Dk. Hamid Hafna Daud
Mkuu wa Kitengo cha fasihi,
Chuo cha Aynu Shams-Cairo.**

Ama Sunna (Hadith), ni lazima ziwe zimepokewa sahihi na watu wa kweli na waaminifu wasioweza kumsingizia uongo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.).

Jambo jingine tunalolipata kutokana na maneno hayo yenyeheki-ma ni kwamba, misingi hii miwili iko juu zaidi kuliko kukosole-wa, kuinyoosha, kuirekebisha na kuipiga msasa. Ama kisi-chokuwa misingi hiyo lazima kikubali kupimwa kwenye mizani ya kukosolewa na tutumie pia akili zetu na tupime kwa mizani ya maneno mpaka tutofautishe kati ya nzuri na mbaya, ya kweli na iliyopotoka.

Nasi katika hali hiyo, hatubabaishwi na anayesema hata awe na cheo na daraja kiasi gani kwa watu, kwani makusudio kwetu ni ukweli tu na neno la haki, hakuna zaidi ya hii hata kama atakayesema ni mmoja kati ya Maswahaba wa Mtume (s.a.w.) kwa sababu hao Maswahaba, kadri ya daraja ya uadilifu na udhibiti walio kuwa nao wa kuhifadhi maneno ya Mtume (s.a.w.), lakini yawezekana kwao kufanya yale wayafanyayo wanadamu wengine kama vile kukosea na kusahau, kwani miyoni mwao kuna wenye makosa, kuna wasio na makosa, kuna wenye nia njema na imani safi na kuna ambao waliokuwa wanafiki waliotokea katika umma kwa mujibu wa maelezo ya Qur'an: "**Na waliokuwa pembezoni mwako ...**" (**Tawba:1-3**).

Hiyo siyo kwamba ilitufanya imani yetu juu ya Maswahaba ilegelege, au msimamo wetu udhoofike juu ya hao waliobeba bendera ya ujumbe mkuu, bado ni kwa kuwa hakuna watu wowote duniani ila kutakuwa katika jamii zao na watu kama hawa, yaani kuanzia wema waadilifu hadi mabaradhuli wanafiki.

Hayo yamethibitishwa kwenye mlingano wa historia na huungwa mkono na 'kanuni za takwimu' katika kusoma jamii ya wanadamu tangu Nabii Adam mpaka leo hii, isipokuwa utaratibu wa kulin-

gania dini ya Mwenyezi Mungu ndiyo umefikia kikomo chake kwa Mtume na Swahaba zake.

Hapakuwa na Mtume aliyekuja na yaliyo matukufu zaidi kuliko ya Mtume (s.a.w.) na hapajatokea watu waliokuwa na maazimio ya kweli na idadi kubwa kuliko Maswahaba zake, Mtume alikuwa ni kielezo cha ukalimifu kwa kuishia kwake ujumbe wa dini na ukamilifu wa dhati yake, ye ye ni bwana wa Mitume na Imam wao, Vilevile ukamilifu wa Qur'an ambayo imekusanya sharia zilizokuja kabla yake.

Pia ukamilifu wa Maswahaba zake kwa kuwa wao waliifuata zaidi kuliko wale wa Mitume 'Ulul A'zmi'⁴ Mtume (s.a.w.) amesema: "Kila Nabii amepewa walioamini katika watu ila mimi nimepewa Qur'an hii na natarajia kwa hiyo wengi wenye kuifauta."

Lakini ukalimifu huu waliojulikana nao Maswahaba wa Mtume haina maana kuwa hakukuwa na wengine walioacha kushikamana na aliyokuja nayo Mtume (s.a.w.) ya uongofu.

Ubora huu wa kuwa Swahaba siyo aina mojawapo ya kuwa mwaminifu wala haukuepukana na kuficha ukafiri wa kudhihirisha Uislamu, licha ya lengo la Mtume (s.a.w.) la kuongoza watu wote alivyotarajia kuwapeleka watu wote kwenye njia ya Mwenyezi Mungu, moyoni mwake na kufuata njia ya kuwapeleka kwenye kuhakikisha kuwa wanaongoka bila ya kumwacha mtu ye yote. Mwenyezi Mungu ameashiria mahali pengi, kama alivyosema:

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكَّرٌ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيْطِرٍ

"Na wakumbushe kwani wewe ni mkumbushaji tu, si mtenzaji nguvu." (Ghashiya:21-22).

4. Ulul A'zmi katika Mitume ni: Nuh, Ibrahim, Musa, Isa na Muhammad (s.a.w.).

Au Aya nyingine:

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهَتَّدِينَ ﴿٢١﴾

“Wewe huwezi kumuongoza umtakaye, bali Mwenyezi Mungu humuongoza amtakaye.” (Al-Qasas : 56).

Na Aya nyingi nyinginezo zinazoashiria jinsi alivyofanya bidii kiongozi huyu mkuu na alivyokuwa na hamu ya kutaka kuongoza watu wote, na jinsi alivyowahurumia kwa kufuata njia isiyo ya uongofu.

Mwenyezi Mungu amemsifu Mtume wake jinsi alivyokuwa ni mfano katika kulingania dini akasema:

“Kwa hakika wewe u mwenye tabia tukufu.”

Na akamliwaza kutokana na pale ambapo hakuweza kuongoza watu wote na alivytarajia kuwaokoa kutokana na upotevu na ukafiri na giza la ujinga kwa kumpa visa vyta ndugu zake Mitume waliotangulia, na huo ndio mwenendo wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe vyake.

“(Hiyo ndiyo) kawaida ya Mwenyezi Mungu iliyotangulia zamani, hutapata mabadiliko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu.”

Yote haya ni ya nguvu kuonyesha kwamba utukufu wa Uislamu u katika misingi yake na si katika watu wake, na kwamba utukufu wake huathiriwa na watu hata wakifanyaje katika kuunga mkono au kuuvunja.

Nami nasema hivi: “Lau binadamu wote na watu wengine kama wao wanglikusanyika wakaishika misingi yake, basi wasinge-

liongeza utukufu wa Uislamu zaidi ya Uislamu wake. Siri ya Uislamu ni katika Misingi yake, na siri ya misingi yake ni misingi yenye na siyo watu.

Na wanaolielewa hili ni wale waliozama kwenye elimu, kwa hivyo Uislamu haudhuriki kwa hali yoyote ile kutoana na kuwakosoa Maswahaba au watafiti wachunguze maneno yao na sera za maisha yao, bali Uislamu ambao umeweke misingi ya uadilifu katika kuhukumu na misingi ya baina ya watu unaruhusu kukosoa huko na kuchunguza, bali umehimiza maadamu ukosaji huo una lengo la kujua ukweli na kupelekea kwenye njia ya sawa.

Msuluhishi mkuu, Mtume (s.a.w.) ametuwekea utaratibu huu wa usawa katika hukmu kwa watu wote, wakati alipotuhimiza kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja tushikamane na neno la haki bila ya kuangalia watu, na tuinusuru haki kama iko kwenye upande dhaifu, na kupinga batili hata kama iko kwenye upande wenye nguvu na tusitofautishe baina ya mtukufu na duni katika kuetkeleza ahadi za Mwenyezi Mungu.

Imetajwa katika Hadith sahihi kwamba Usama bin Zaid (kipenzi cha Mtume) alimuombea kwa Mtume mwanamke mwizi aliyeiba aliyetokana na koo zinazoheshimika za Maquireishi, lakini Mtume alikataa ikawa lazima huyo apigwe haddi, mara akasema: “Enyi watu, kwa hakika waliokuwa kabla yenu waliangamia kwani ilikua wanapoiba mtukufu wao humwacha bila ya kumwadhibu na anapoiba mnyonge humpiga haddi, naapa kwa Mwenyezi Mungu, lau hata Fatma bint Muhammad angeliiba, ningelimkata mkono wake!”

Hivi ndivyo alivyokataa Mtume Muhammad (s.a.w.), muasisi wa uadilifu na usawa duniani, kuwacha kumpiga haddi mwanamke wa kabilia la Makhzum hata kama nasaba yake ilikuwa tukufu kiasi gani.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhangaa wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swalaa
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi

-
25. Yajue Madhehebu ya Shia
 26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
 27. Al-Wahda
 28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
 29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
 30. Mashukio ya Akhera
 31. Al Amali
 32. Dua Indal Ahlul Bayt
 33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
 34. Haki za wanawake katika Uislamu
 35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
 36. Kumswalia Mtume (s)
 37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
 38. Adhana.
 39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
 40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
 41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
 42. Kupaka juu ya khofu
 43. Kukusanya swala mbili
 44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
 45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyga
 46. Kusujudu juu ya udongo
 47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
 48. Tarawehe
 49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
 50. Kupunguza Swala safarini
 51. Kufungua safarini
 52. Umaasumu wa Manabii
 53. Qur'an inatoa changamoto

-
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
 55. Uadilifu wa Masahaba
 56. Dua e Kumayl
 57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
 58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
 59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
 60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume
 Muhammad (s)
 61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
 62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
 63. Kuzuru Makaburi
 64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
 65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
 66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
 67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
 68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
 69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
 70. Tujifunze Misingi Ya Dini
 71. Sala ni Nguzo ya Dini
 72. Mikesha Ya Peshawar
 73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
 74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio
 njia iliyonyooka
 75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
 76. Liqaa-u-llaah
 77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
 78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
 79. Uislamu Ulienea Vipi?
 80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)

-
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
 82. Urejeo (al-Raja'a)
 83. Mazingira
 84. Utokezo (al - Badau)
 85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
 86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
 87. Uislamu na Uwingi wa Dini
 88. Mtoto mwema
 89. Adabu za Sokoni
 90. Johari za hekima kwa vijana
 91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
 92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
 93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
 94. Tawasali
 95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
 96. Hukumu za Mgonjwa
 97. Sadaka yenyе kuendelea
 98. Msahafu wa Imam Ali
 99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
 100. Idil Ghadiri
 101. Kusoma sura zenyе Sijda ya wajibu
 102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
 103. Huduma ya Afya katika Uislamu
 104. Sunan an-Nabii
 105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
 106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
 107. Shahiid Mfiadini
 108. Kumswalia Nabii (s.a.w)
 109. Ujumbe - Sehemu ya Kwanza

-
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
 111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
 112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
 113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
 114. Hadithi ya Thaqalain
 115. Maarifa ya Kiislamu
 116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
 117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
 118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
 119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
 120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
 121. Safari ya kuifuata Nuru
 122. Fatima al-Zahra
 123. Myahudi wa Kimataifa
 124. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
 125. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
 126. Visa vya kweli sehemu ya Pili
 127. Muhadhara wa Maulamaa
 128. Mwanadamu na Mustakabali wake
 129. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Kwanza)
 130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Pili)
 131. Khairul Bariyyah
 132. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
 133. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
 134. Yafaayo kijamii
 135. Tabaruku
 136. Taqiyya

-
137. Vikao vya furaha
 138. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
 139. Visa vya wachamungu
 140. Falsafa ya Dini
 141. Kuhuzunika na Kuomboleza - Azadari
 142. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
 143. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
 144. Kuonekana kwa Allah
 145. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Kwanza)
 146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Pili)
 147. Ndugu na Jirani
 148. Ushia ndani ya Usunni
 149. Maswali na Majibu
 150. Mafunzo ya hukmu za ibada
 151. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
 152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
 153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
 154. Abu Huraira
 155. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
 156. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
 157. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
 158. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
 159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
 160. Qur'ani Tukufu - Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
 161. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
 162. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
 163. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu

-
164. Uislamu Safi
 165. Majlisi za Imam Husein Majumbani
 166. Mshumaa
 167. Uislam wa Shia
 168. Amali za Makka
 169. Amali za Madina
 170. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
 171. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
 172. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
 173. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
 174. Umoja wa Kiislamu na Furaha
 175. Mas'ala ya Kifiqhi
 176. Jifunze kusoma Qur'ani
 177. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
 178. Hayya 'Alaa Khayri'l-Amal Katika Adhana
 179. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
 180. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
 181. Uadilifu katika Uislamu
 182. Mahdi katika Sunna
 183. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
 184. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
 185. Abu Talib - Jabali Imara la Imani
 186. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
 187. Vijana na Matarajio ya Baadaye
 188. Usalafi - Historia yake, maana yake na lengo lake
 189. Ushia - Hoja na Majibu
 190. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
 191. Maombolezo - Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)

-
192. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
 193. Takwa
 194. Amirul Muuminina ('as) na Makhalfifa
 195. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (a.s.)
 196. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu
 197. Mtazamo kuhusu msuguano wa kimadhehebu
 198. Upotoshaji Dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
 199. Nchi na Uraia - Haki na wajibu kwa Taifa
 200. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah kwa Imam Ali (a.s.)
 201. Uongozi wa kidini - Maelekezo na utekelezaji wa Kijamii

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

Back Cover

"Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao. Na Mwenyezi Mungu atakamilisha nuru yake ijapokuwa makafiri watachukia." (Qur'an 61:8)

Baadhi ya waumini wema na wenyewe nia nzuri na wanao-jishughulisha kuondoa hitilafu zilizoko mionganini mwa umma wa Kiislamu walimuomba mwandishi wa kitabu hiki akusanye maoni ya baadhi ya waandishi wa kisasa kuhusu umoja wa umma wa Kiislamu ili kutekeleza kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakane."**

Vilevile kujiepusha na mizozo kwa kauli yake Mwenyezi Mungu: **"Wala msizozane mtafeli ..."**

Katika hali kama hizi za sasa za kiubaguzi, yapasa Waislamu wote wawe bega kwa bega, wawe kitu kimoja na wafanye juhudzi za kuungana na kuwa na sauti moja ili lao liwe moja dhidi ya maadui wao.

Mwenyezi Mungu (s.w.t.) anasema: **"Hakika umma wenu huu ni umma mmoja na Mimi ni Mola wenu basi niabuduni"**

Ikiwa madhehebu nyingine potofu hivi leo zinaungana kwa wingi, kwa nini basi sisi Waislamu tusiwe na umoja na tusihurumiane?

Ndani ya kitabu hiki utakuta maoni yanayo husu Umoja wa Waislamu yaliyotolewa na wanachuoni wakubwa na mashuhuri wa Shia na Sunni.